ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Soud Yussuf Mgeni	Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Wawi.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.

23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Omar Ali Shehe	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Chake-Chake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Abass Juma Muhunzi	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Chambani.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Jimbo la Mkanyageni.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Said Ali Mbarouk	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Gando.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.

47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
49.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
53.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
55.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
57.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
58.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
59.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
60.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
61.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
62.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
63.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
64.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
65.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.

67.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
68.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
70.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
71.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
73.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
74.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
75.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.
76.Mhe. Zahra Ali Hamad	Nafasi za Wanawake.
Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nne – Tarehe 26 Januari, 2009

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini Zanzibar na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Said Ali Mbarouk (Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi) Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani maombi ya kambi ya upinzani juu ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana nayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 86

Zanzibar Kujiunga na *OIC*

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Kwa kuwa Zanzibar iliwahi kujiunga na umoja wa nchi za Kiislam duniani (*OIC*), kwa lengo la kujikwamua kiuchumi kutokana na misaada ya kiuchumi inayotolewa na jumuiya hiyo. Pia kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliitaka Zanzibar ijitoe katika umoja huo, ili itoe nafasi kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ijiunge na hatimae Zanzibar ipate nafasi ya kujiunga. Na kwa kuwa muda umeshakuwa mkubwa tokea Zanzibar ijitoe katika jumuiya hiyo yaani zaidi ya miaka kumi, huku bado Serikali ya Jamhuri ya Muungano haijajiunga na umoja huo.

(a) Je, serikali ina mpango gani wakujiunga tena na jumuiya hiyo.
(b) Je, Mhe. Waziri, huoni kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haina nia ya kujiunga na jumuiya hiyo.
(c) Kwa kiasi gani Zanzibar ingefaidika iwapo ilijiunga zaidi ya miaka kumi iliyopita.

Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi - Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 86 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa maelezo ya ufafanuzi kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mgawanyo wa majukumu ya serikali zetu mbili kulingana na hati ya masuala ya muungano na masuala ya mambo ya nje ni suala la Muungano. Uanachama katika Mashirika mbali mbali ya Kimataifa likiwemo lile la Jumuiya ya Nchi za Kiislamu (*OIC*) ni suala la mambo ya nje ambapo Serikali ya Muungano ndiyo yenye jukumu la kuomba uanachama huo. Zanzibar haijawahi kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Nchi za Kiislamu Duniai, bali ilianzisha mchakato wa kuomba kuwa mwanachama wa jumuiya hiyo. Hata hivyo, zoezi hilo lilibidi kusimama kutokana na sababu za kikatiba kama nilivyoeleza hapo awali.

Mhe. Spika, suala la Zanzibar kujiunga na *OIC* peke yake lilijadiliwa katika vikao mbali mbali vya serikali zetu mbili na kukubalika mambo yafuatayo:-

i. Zanzibar isitishe mchakato wake wa kuomba uanachama katika jumuiya hiyo .
ii. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iangalie badala yake uwezekano wa kujiunga na jumuiya hiyo kwa madhumuni ya kukidhi matakwa ya kikatiba. Kwa Zanzibar kutokuwa mwanachama wa *OIC* katika kipindi chote cha miaka zaidi ya kumi. Naomba kukiri kuwa hili ni swali ambalo lingeweza kujibika vizuri kwa kutumia takwimu kama zingekuwepo. Kwa kuwa hatuna takwimu za aina hiyo sio busara kujibu kifungu hiki, kwa kutumia hisia zangu tu.

Mhe. Spika, hata hivyo naomba kulijuilisha Baraza lako tukufu kuwa nchi inapoamua kujiunga katika Taasisi au Jumuiya za Kimataifa huangalia zaidi maslahi itakayoweza kuyapata kutokana na uanachama wake. Kama ilivyo kwa Jumuiya nyengine za Kimataifa, Jumuiya ya *OIC* inayo madhumuni na malengo yake kwa wanachama wake. Kutofaidika na malengo hayo ndiko kwa sasa tunakoweza kusema kuwa Zanzibar haikufaidika ingawa ni vigumu kusema kwa kiasi gani.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Wazanzibari tuko Waislamu asilimia 90 na kuendelea na wenzetu Tanzania Bara wako Wakiristo asilimia 90 na kuendelea. Mhe. Spika, katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano bado haijaiweka bayana kama masuala ya kidini yamo kwenye muungano. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anitafsirie ni nini kitakachokuwa kikwazo jambo hili likawa sasa hivi lazima lishughulikiwe kimuungano na sisi kwenye mambo ya dini bado hatujaona kama ni ya muungano.

Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa upande mmoja nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba Zanzibar Waislamu tuko karibu asilimia 98 sio asilimia 90. Mimi sikubaliani na kwamba Tanzania Bara asilimia 90 ni Wakiristo, hilo suala hajafanya utafiti wa kutosha. Kimsingi ni kwamba sina takwimu sahihi, lakini labda ni asilimia 60 sio asilimia 90.

Mhe. Spika, sasa naomba nimjibu swali lake Mhe. Mwakilishi kuhusu Zanzibar kutaka kujiunga na *OIC* na kwa kuwa tuko asilimia 90 ni suala la kidini na kwa nini likaingizwa katika suala la muungano.

Mhe. Spika, kimsingi ni kwamba Zanzibar ilipojiunga na *OIC* haikujiunga kwa madhumuni ya kidini, Zanzibar ilipoomba mchakato wa kutaka kujiunga na *OIC* ilifanya madhumuni yale kwa lengo zaidi la madhumuni ya kiuchumi na sio kwa madhumuni ya kidini. Kwa sababu Wazanzibari kama alivyosema mwenyewe zaidi ya asilimia 90 ni Waislamu kwa hiyo kulikuwa hakuna haja ya kutafuta jumuiya nyengine ya kuongezea Uislamu tuliokuwa nao. Lakini tuliamua kuingia katika mchakato huu kwa ajili ya jumuiya ile na malengo yake makuu zaidi ni ya kiuchumi.

Kwa vile tumeona nchi nyingi ambazo zilizojiunga na Jumuiya hii ya *OIC* pamoja na kwamba sio za Kiislamu lakini zimeweza kufaidika na kuweza kupata maendeleo makubwa ya kiuchumi na ya kijamii. Kwa hivyo, kimsingi ni kwamba suala hili linahusu mambo ya nje, ndio Zanzibar ikabidi tuingie Jamhuri nzima ya Muungano. Kwa hatua ambayo iliyofika sasa hivi kupitia mijadala mbali mbali katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na kauli ya Mhe. Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, suala hili baada ya kufanyiwa utafiti limeonekana halina athari yoyote na tunategemea pengine wakati wowote wenzetu watatoa tamko la kuanza kujiunga na hiyo jumuiya.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, asubuhi hii na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali muhimu la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wakati anajibu amezungumzia kwamba ameingiza suala la mambo ya nje kuwa ni la muungano.

a) Je, anafahamu kwamba suala la mambo ya kiuchumi halihusiani na muungano, na ikiwa hivyo ndivyo suala la kuwa Jamhuri ya Muungano imetaka tujitoe na wao wakawa hawajajiunga mpaka sasa hivi inaonesha ni nia njema kwa upande wetu sisi kutuangusha hasa kiuchumi.

b) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haioni kwamba hii ni kasoro kubwa katika muungano na ni jambo la kushughulikiwa mara moja.

Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, suala la kiuchumi ni kwamba kimsingi *OIC* tumeamua kujiunga na jumuiya moja kwa moja tofauti kama ingelikuwa tumepeleka maombi ya kuomba msaada vitu hivyo kidogo vingelikuwa viko tofauti, lakini sisi tumeamua kujiunga ina maana tayari tumekuwa ni wanachama. Kwa hivyo, moja kwa moja suala la kujiunga na Jumuiya ya *OIC* ni suala la muungano.

Mhe. Spika, kimsingi ni kwamba kwa kiasi fulani suala hili lina ukweli ndani yake, kwa sababu limetuathiri kwa kiasi fulani kwani kama tungeliweza kujiunga na jumuiya hii karibu zaidi ya miaka 10 iliyopita tungelikuwa tumeshapiga hatua kubwa sana za maendeleo. Vile vile kuna siku niliwahi kulizungumza hili suala kwamba mfano, kama sisi katika hiyo misaada ambayo *OIC* ingelitupa, basi tungelisema tupatiwe matrekta 50 nadhani tungekuwa tumepiga hatua kubwa sana ya kiuchumi lakini ni kwamba fursa hii mpaka leo bado tumeikosa.

Kama nilivyosema kwamba suala hili mpaka hivi sasa tulipozungumza na Waziri wa Mambo ya Nje bado suala hili lina uwezekano mkubwa karibu kwa asilimia 80, na ile mijadala ambayo imejitokeza pale kati kati kwa wale wanazuoni waliokuweko kule Bara, yale ilikuwa ni mambo yao ya nje ya kidini kwa sababu pale suala lililokuwa linazungumzwa ni lile lililozungumzwa Bungeni wale walilichupia tu, lakini ilikuwa sio suala lao hasa. Ndio maana Waziri wa Mambo ya Nje akasema hao wanazuoni waache wabishane lakini Wabunge wenyewe ndio watakaoamua.

Mhe. Spika, labda nijaribu kuzungumzia hisia zetu. Ni kwamba iwapo mfano wenzetu hawatofikia pahala kwamba Tanzania kujiunga na jumuiya hii basi sisi kama Zanzibar tutaomba fursa tuingie kama Zanzibar peke yetu, kwa sababu Katiba ya muungano ni zaidi, na muungano wetu ni kwa manufaa ya wananchi wa pande mbili zote za muungano. Bado hakuna utafiti mpaka sasa hivi ulionesha kwamba kujiunga na Jumuiya ya *OIC* kuna athari zozote za kidini au za kiuchumi. Kwa hiyo, kubwa kilichokuwepo ni kwamba sisi tunategemea tutaweza kujiunga na *OIC*. Mhe. Spika, huo ndio msimamo.

Mhe. Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kutoa maelezo ya ziada kwa pale alipomalizia Mhe. Waziri namshukuru sana kwa maelezo yake.

Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi katika suala lake amesema kwamba masuala ya uchumi si masuala ya muungano na kwa makubaliano ya muungano ni kweli suala la uchumi moja kwa moja linaonekana hata ukiangalia Katiba haliko katika orodha ya mambo ya muungano. Lakini ni kwamba yapo mashirika ya kimataifa na zipo nchi zinaposhirikiana na nchi fulani katika masuala ya kiuchumi haziweki masharti ya utaifa.

Kwa mfano, yapo Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Shirika la Afya Duniani halina masharti hayo ni kwamba Zanzibar imekuwa ikipata misaada hiyo kwa kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, *UNICEF*, *UNESCO*, *UNFPA* haya ni masharika ya Umoja wa Mataifa ambayo hayana sharti la utaifa hata nchi isiyokuwa na utaifa wa moja kwa moja kama ilivyo Zanzibar inayo haki ya kupata fursa za kiuchumi na misaada mbali mbali, na kwa muda mrefu zaidi miaka 45 Zanzibar imekuwa ikinufaika na masuala hayo.

Mhe. Spika, pia zipo nchi moja moja kubwa na ndogo, maskini na matajiri zimekuwa zikishirikiana na Zanzibar na kutoa misaada mbali mbali ya masuala ya uchumi, lakini kwa utaratibu ambao hakuna masharti yakuwa na utaifa. Katika siku za karibuni kumeanza utaratibu, kwa mfano wafadhili ambao wanasema kwamba wanatoa misaada Tanzania kwa kupitia misaada ya kibajeti, na misaada hii moja kwa moja inakuja katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar imekuwa ikipewa asilimia 4.5.

Mhe. Spika, sasa tukija kwenye suala lako kuhusiana na *OIC*. *OIC* ni taasisi ambayo kwa upande mmoja kuna masuala ya kidini lakini kwa upande mwengine kuna masuala ya mahusiano ya kiuchumi. Kwa mnasaba huo ukiangalia Katiba na utaratibu wanaoutumia *OIC* ni kwamba wao hawana utaratibu kama ule niliouleza wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa kwamba wanaweza kushirikiana na nchi ya kawaida ambayo hata kama haina utaifa. Hawa ukiangalia utaratibu wao inaonekana wazi kuna masharti nchi wanachama zinazojiunga ni nchi ambazo zina utaifa.

Kwa maana hiyo, kwa utaratibu wetu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaposhirikiana na nchi nyengine ambazo zinahitaji masuala ya taifa au mashirika, kwa maana hiyo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio maana inafanya kazi hiyo. Ndio maana kwa muda mrefu imekuwa ikiambiwa kwamba Zanzibar inapotaka kujiunga kwenye suala hili kuwe na mashauriano ya karibu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu kuna sharti hilo la utaifa, ambalo utaifa sio mali ya Zanzibar peke yake, lakini pia si mali ya

Tanzania Bara peke yako ni mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo Bara na Visiwani.

Kwa hivyo, tunapotaka kufanya jambo hilo lenye masharti hayo tukae, tushauriane na tuelekezane na kama tunaona kuwa jambo hili lina maslahi ya kiuchumi au kijamii kwa upande fulani, basi jambo hilo tukubaliane. Ndio maana tunasema yamekuwepo mazungumzo ingawa katika siku za karibuni jambo hili limeleta hisia kubwa katika Bunge na sehemu nyengine. Mimi nasema kwa maoni yangu jambo hili linapaswa kufanyiwa kazi kwa umakini wa hali ya juu, na busara itawale zaidi katika jazba kwa sababu ni jambo ambalo kwa upande mwengine kuna masuala ya kidini, kwa upande mmoja masuala ambayo wakati mwengine imani za watu zinaleta misuguano isiyokuwa ya lazima sana. Nasema jambo hili kama sisi Zanzibar tunahisi ni jambo ambalo lina maslahi makubwa ya uchumi. Mimi nadhani tuendelee kujenga hoja hiyo na tutumie busara kulijadili na *inshaallah* nafikiri tukifanya hivyo bila shaka njia itapatikana. Mhe. Spika, nakushukuru.

Nam 70

Utaratibu wa Kuharakisha Kesi

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Kny: Mhe. Anaclet Thobias Makungila) - Aliuliza:-

Wizara ya nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kwa kushirikiana na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ina utaratibu gani wa kuimarisha mfumo wa uendeshaji wa mashtaka kwa kujenga utaratibu wa kukamilishwa upelelezi kabla ya kufunguliwa mashtaka ili kupunguza usumbufu usio wa lazima kwa kisingizio cha ushahidi haujakamilika wakati mashtaka yameshafunguliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 70 kama ifuatayo:-

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika kuimarisha mfumo wa uendeshaji wa mashtaka na kujenga utaratibu wa kukamilisha upelelezi kabla ya kufunguliwa kesi imechukua hatua mbali mbali katika kufanikisha utaratibu huo na hatua hizo ni kama zifuatazo:-

- Kabla ya kuanza kutekeleza mpango/mkakati huo afisi ilifanya mazungumzo na Wakuu wa Upelelezi wa Jinai wa Mikoa yote ya Unguja kupitia vikao vyake vya kila mwezi vinavyofanywa kati ya

Mkurugenzi wa Mashtaka na Polisi. Kupitia vikao hivyo, imekubalika na kusisitizwa kwamba kesi zisifunguliwe kabla ya upelelezi kukamilika.

- Wanasheria wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka wamefanya na wanaendelea kufanya ziara za kutembelea vituo vya polisi kutoa elimu na kusisitiza mkakati wa kufanya upelelezi kabla ya kesi na umuhimu wa kufanya hivyo.

- Mkakati mwengine ni kutozifungua Mahakamani kesi zote za jinai zilizokuwa hazijakamilishwa upelelezi isipokuwa kwa kesi maalum ambazo Mkurugenzi wa Mashtaka atatoa maelezo kufunguliwa kesi hizo au kama kuna mazingira ambayo yataathiri hatma ya kesi husika.

- Kwa kuhakikisha mkakati wa kupeleleza kesi kwanza kabla ya kufunguliwa unatekelezwa kesi yoyote inayotokea Mahakamani kutoka polisi hupitiwa/kufanyiwa tathmini ushahidi wake na ikionekana ushahidi huo kuwa hautoshelezi kesi hiyo haifunguliwi. Jalada husika hurejeshwa kwa polisi likiwa na maelekezo au mapendekezo ya kufanyiwa upelelezi zaidi au kurekebishwa baadhi ya makosa.

Kutokana na taratibu hizo zilizotajwa, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imefanikiwa kupunguza idadi kubwa ya kesi zisizokuwa za msingi na si lazima kufunguliwa kabla ya kupelelezwa

Aidha, imepelekea kuongeza ufanisi wa kuziendesha kesi na kupunguza usumbufu kwa wananchi ukilinganisha na kabla ya utaratibu wa kupeleleza kesi haujaanza kutekelezwa.

Mhe. Spika, hapa kuna mifano michache inayoonesha maendeleo hayo. Kwa mfano, katika Mahkama ya Mkoa Vuga kesi zilizofunguliwa kwa mwaka 2006 ni 423, mwaka 2007 kesi 299 na mwaka 2008 kesi 210. Pia kwa kesi za watoto (*juvenile*) kesi zilizofunguliwa 2006 ni 60, 2007 kesi 11 na 2008 kesi 10. Kwa upande wa kesi za Mahakama ya Wilaya ya Mwanakwerekwe kesi zilizofunguliwa kwa mwaka 2006 zilikiwa 1534, mwaka 2007 kesi 534 na mwaka 2008 kesi 412.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, kwanza naipongeza Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kuanzisha utaratibu huu ambao kwa kiasi fulani utawapunguzia watu usumbufu.

Mhe. Spika, ni kwamba polisi wamemtuhumu mtu na wakawa wamo katika utaratibu wa kufanya upelelezi, lakini mtu yule alituhumiwa akakamatwa na yuko mahabusu na kesi haiwezi kupelekwa Mahakamani mpaka upelelezi ukamilike kwa utaratibu huu mpya.

Je, kwa sheria pia inawataka polisi wamuweke mtu pale mahabusu kwa masaa yasiozidi 48, lakini upelelezi huo siku nyengine unaweza ukachukua mwezi mzima, sasa polisi wana mkakati gani kwamba yule mtu wataendelea kumuachia huku wakifanya upelelezi au watamuweka mwezi mzima pale.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza namshukuru sana kwa pongezi alizozitoa kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuwa inafanya kazi vizuri. Pili ni kwamba wakati mtuhumiwa anapotuhumiwa na polisi wakamuweka ndani kuna suala la dhamana, dhamana kwa kesi ambazo zinazohitajika kuchukuliwa dhamana bila shaka atatokea mtu atamchukulia dhamana, ikiwa hakutokea mtu wa kumchukulia dhamana bila shaka atakuwa amekaa ndani.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Katika utaratibu huu ambao unaonekana kuwa ni mzuri. Je, hautotoa mwanya kwa wahalifu wanaotuhumiwa kuweza kutoroka kwa sababu bado kushtakiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, maana ya kutokea mtu kumchukulia dhamana ni kuhakikisha kwamba mshtakiwa yule atamshughulikia ili asitoroke, akitoroka ile dhamana itakuwa inachukuliwa hatua zake za kisheria.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nampongeza kwa kutupa taarifa kwamba hili tatizo limepungua. Pamoja na kupungua bado kuna tatizo kama hili lakini lina sura nyengine tatizo la watu kukamatwa ovyo pengine bila ya kuwa na sababu za msingi na huwekwa polisi na baadae huachiwa bila ya kupelekwa Mahakamani, hili linafanana na hilo lililokuwepo.

Mhe. Spika, haoni kwamba Mhe. Waziri ipo haja ya kuelimisha hasa Wakuu wa Wilaya kuacha tabia hii ya kutoa amri ya kukamatwa watu ovyo wakasumbuliwa bila ya kuwa na makosa yoyote.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, namshukuru vile vile kwa pongezi ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na utaratibu wake mpya. La pili Mhe. Spika, ni kwamba tunahitaji viongozi sote kuwa macho na tabia za kibinadamu ambazo hivi sasa zinatokea katika maeneo

mengi, tabia za kubandikizana kesi ni vizuri tuwe macho katika suala hili na tuwe tunatoa taarifa na kufuatilia kwa undani masuala haya kwa sababu ofisi hairuhusu watu kubandikizwa kesi na kuwekwa ndani bila ya tatizo lolote. Kwa hivyo, mkakati mwengine ni kwamba Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka inawaeleza watu wa vituo vya polisi na mambo mengineyo ili waache tabia ya kuwabambikizia watu kesi. Hili ni suala la kushirikiana sote kwa pamoja.

Nam. 15

Uimarishaji wa Kitengo cha Ujenzi katika Kikosi cha KMKM

KMKM ni miongoni mwa taasisi za serikali zinazofanya vizuri sana hasa katika sekta ya ujenzi wa majengo ambapo taasisi hiyo imeweza kujenga majengo ya kisasa kabisa kama vile Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Ikulu ya Wete, Pemba na kwa bei nafuu sana ukilinganisha na kampuni nyengine za ujenzi hasa zile za binafsi.

a) Serikali ina mipango gani ya kuhakikisha kwamba angalau majengo yote ya serikali yanajengwa na kikosi hiki ili kukiwezesha kujiimarisha kifedha na vile vile kuokoa fedha nyingi za serikali ambazo zingetumika kwa kampuni za binafsi katika ujenzi wa majengo.

b) Kwa kuzingatia kwamba kikosi kina mhandisi mmoja angalau tu mwenye sifa, wizara ina mpango gani wa makusudi wa kuhakikisha inasomesha vijana wengi zaidi katika fani ya ujenzi ili waweze kukisaidia kikosi katika shughuli za ujenzi na kuweza kushindana na kampuni nyengine kubwa ndani na nje ya nchi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 15 lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu napenda kwanza kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa vikosi vyetu vyote vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni taasisi zinazofanya kazi vizuri sana katika sekta ya ujenzi wa majengo mbali mbali. Kwa msingi huo, ndio sababu ya kushirikishwa kikamilifu katika kuendeleza ujenzi wa Nyumba za Maendeleo Michenzani.

a) Mhe. Spika, ukiacha majengo ambayo yanajengwa na Idara ya Majenzi, mejngo mengine yote ya serikali mapya au yanayofanyiwa matengenezo yanajengwa na moja kati ya vikosi

vyetu vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Huo ndio mkakati uliopo. Mfano hai ni ujenzi wa Afisi za Wabunge Vikosi vya SMZ ndivyo vilivyopewa kandarasi ya kujenga ofisi hizo.

b) Suala la kuongeza ujuzi kwa wataalamu wakiwemo hawa wahandisi wa ujenzi lipo chini ya dhamana ya kikosi chenyewe. Serikali iko tayari kutoa msaada pale unapohitajika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake sahihi kuwa vikosi vyetu vya SMZ vina ushindani mkubwa katika utekelezaji wa majengo na katika sehemu mbali mbali za nchi yetu. Lakini pili nimpongeze kuwa vijana wetu hao wana nidhamu ya kutosha hasa ya kiuaskari katika utekelezaji wa kazi zao.

Je, kwa kuwa Nyumba za Maendeleo za Michenzani kwa asilimia kubwa wameshiriki katika uejnzi mpaka zilikakamilika, na kwa kuwa hivi sasa baadhi yao wanaendelea na nyumba za Mpapa, huko Bambi. Mhe. Waziri ana mpango gani angalau wale watendaji wazuri au mafundi wazuri zaidi, kama vile katika ushindani wa riadha kuna wa kwanza, wa pili na watatu akawatunuku zawadi angalau ya vyeo kama ukoplo, *lance corporal* au *sergeant* na vyeo vyenginevyo kwa wale waliofanya vizuri zaidi?

Mhe. Spika: Swali limetoka kwenye ujenzi wa majumba na ufanisi mzuri sasa tunataka tujenge hiyo *human resource* yenyewe.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, kwa ukweli kazi na utaratibu unaofanywa na vikosi vyote vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pale kijana au mpiganaji anapoweza kufanya kazi nzuri basi huwa anapewa cheo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza yenye a, b na c.

a) Mhe. Spika, kwa kuwa KMKM ni kikosi ambacho kinazuia magendo yasitokee hapa nchini, na kwa kuwa muangaza mbili moja humpona je, Mhe. Waziri haoni ujenzi na kuzuia magendo moja litawapona?

b) Kwa kuwa ajira hapa Zanzibar ni kidogo, huoni kuzikumbatia ajira mbili sehemu moja ni tatizo?

c) Kwa kuwa karafuu bado zipo nyingi haoni ni kuwaachia kusafirisha kiholela KMKM kwa kushughulikia ujenzi?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, Kikosi cha KMKM ni kikosi ambacho utekelezaji wake wa kazi unasifikana na unajulikana, pia ni mahodari wa kuzipanga kazi zao zisiingiliane. Wakati wanashughulikia magendo wapo wanaoshughulika na magendo, wakati wa ujenzi unapoendelea wapo wanaoshughulika na ujenzi, kitu muhimu ni uwezo wa kuweza kujipanga vizuri na KMKM wanajipanga vizuri kwa shughuli zao zote bila kuwapona.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa taratibu za ujenzi huitishwa kwa *tender* ili kuhifadhi fedha za serikali zisipotee, katika *tender* hutakiwa kampuni tatu zishiriki, hivyo wakati wa kuwashirikisha KMKM wanajenga moja kwa moja au zinakuwa kampuni tatu zimeshindana vikosi vikazidi ndio vikapewa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, namba aliyoitoa Mhe. Ame Mati ni tatu, vikosi vyetu viko vitano kwa hivyo kimoja wapo kitapata kikosi.

Nam. 3

Uanzishwaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii umeanzishwa kisheria kwa lengo la kuwapunguzia usumbufu wafanyakazi wanapofika muda wa kustaafu kazi na kupata mafao yao katika muda muwafaka ili kuwafaa katika maisha yao baada ya kustaafu.

a) Je, Mhe. Waziri unafahamu kwamba kuna upotevu wa vielelezo vya badhi ya wafanyakazi vinavyothibitisha uhalali wa malipo yao?

b) Je, unafahamu kwamba upotevu huo husababisha usumbufu mkubwa kwa wafanyakazi waliostaafu ikiwa ni pamoja na kuchelewa kupata malipo yao?

c) Je, Wizara ina mkakati gani wa kuliondosha tatizo hilo?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi) – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali Nam. 3 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kama Mhe. Mwakilishi alivyofanya masahihisho ni kweli kwamba huu ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na sio Mfuko wa Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba nikubaliane na Mhe. Mjumbe kuwa miongoni mwa madhumuni ya kuanzishwa kwa Mfuko huu ni kuwapunguzia usumbufu wafanyakazi wanapofikia muda wa kustaafu kazi na kupata mafao yao katika muda muwafaka ili kuwafaa katika maisha yao ya baada ya kustaafu.

Napenda nimhakikishie Mhe. Mjumbe kuwa lengo hilo kwa sasa limefikiwa kwa asilimia kubwa kwani madai ya mafao ya wastaafu huchukua kipindi cha wiki tatu hadi nne au siku thalathini za kazi kutoka siku ambazo amekamilisha kufungua madai yake yakiwa na vielelezo vyote. Baada ya maelezo hayo sasa naomba nijibu swali la Mhe. Mjumbe lenye vifungu a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a) Nikiwa kama waziri ninaeshughulikia taasisi hii naelewa kwamba kunajitokeza kasoro, changamoto na mafanikio kwenye kila eneo la utendaji. Suala la upotevu wa kumbukumbu lilikuwa linajitokeza hapo nyuma ingawaje kwa sasa tahadhari kubwa zimechukuliwa na matumizi ya teknolojia ya kompyuta yamesaidia sana katika kupunguza upotevu huo.

(b) Ninafahamu kuwa upotevu unapotokea hata kwa hizo mara chache ulipowahi kutokea husababisha usumbufu kwa wafanyakazi waliostaafu ikiwa ni pamoja na kuchelewa malipo yao na ndio maana nikasema kuwa tunachukua hatua za makusudi za kudhibiti kasoro hizo.

(c) Wizara kwa kushirikiana na taasisi yenyewe imeandaa mikakati mbali mbali ya ziada ya kuondoa kasoro katika hizo zikiwemo za kutumia mifumo ya kisasa ya kutunza kumbukumbu kama vile uwekaji wa kumbukumbu kwa kutumia kompyuta, kuimarisha mbinu za utoaji huduma pamoja na kuwapatia wafanyakazi mafunzo ya utunzaji bora wa kumbukumbu. Mikakati hii kama nilivyosema hapo mwanzo imeanza kudhibiti kasoro ndogo ndogo zilizowahi kutokea.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Kaimu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza.

a) Mfuko huu katika uwekaji wa fedha za wateja wake huwa unafanya biashara, biashara wanayoifanya hivi sasa kubwa wanafanya kwenye majengo na wataalamu wa biashara wanasema majengo katika kurejesha fedha zake yanachukua muda mrefu. Je, haoni kama hiyo ni hatari kwa upande mmoja? Kwa nini wasiweke fedha mabenki ili wakapata faida ya kuweza kupata tija haraka haraka.

c) Katika uwekezaji huo panaingia faida? Je, hawa wateja nao wanapata faida hiyo?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, ni kweli kwamba Mfuko unawekeza katika majengo lakini pia tukumbuke kwamba hata benki Mfuko huu ni mmoja wa wateja wakubwa katika kuwekeza fedha zake.

Kuhusu wateja kama wanapata faida kutokana na uwekezaji huu naweza kusema wanapata kwa sababu fedha zao zinakuwepo na wanalipwa kwa wakati. Kwa mfano mwaka jana tu karibu wateja mia tatu na sita (306) walilipwa shilingi milioni mia tisa na thalathini na sita.

Kwa hivyo, haya ni mafanikio na fedha zao ziko salama ukiachilia mbali miaka ya nyuma ambayo tulikuwa hatuna Mfuko huu wastaafu walikuwa wakichukua muda wa miaka minane mpaka saba bila ya kulipwa. Kwa hivyo, hii ina faida kwa wateja.

Mhe. Mohammed Ali Salim: Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Kaimu Waziri swali moja la nyongeza. Hivi katika huu Mfuko kuna afisa au kitengo kinachohusika na kuhakikisha kuwa hawa waajiri wote wanapeleka fedha za wafanyakazi wao? Kama kiko, kwa nini inatokezea watu kustaafu na ikawa bado kule fedha zao nyengine hazikufika?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, kitengo hiki kipo na kinafuatilia na kuna baadhi ya taasisi za watu binafsi na serikali kidogo wanakuwa sugu katika ulipaji wa madeni haya, lakini kwa mujibu wa sheria wanakuwa wanafuatiliwa na kubanwa ili waweze kuwasilisha mafao ya wafanyakazi wao.

Nam. 28

Madaktari Kutovaa Sare Kazini

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu - Aliuliza:-

Kwa kuwa kutokuwa na sare kazini kunachangia kuwababaisha na kutokujulikana kati ya daktari, muuguzi na mfanyakazi wa kawaida wa hospitali au wa wizara na kwa kuwa sare (*uniform*) ni utambulisho wa kumuwezesha mgonjwa kumjua mtu anayemhudumia ni nani.

(a) Je huoni kwamba kutokuvaa sare kazini kunawapunguzia madaktari wetu hadhi na heshima ya kazi na kunaondoa nidhamu ya kazi.

(b) Kama kutokuvaa sare (*uniform*) ni mazoea ya madaktari wetu, sio utaratibu, kwa nini basi washindwe kuvaa hata vitambulisho vya kazi, kama kuvaa sare kwao ni aibu au wanaona haya.

(c) Je kuvaa sare kunawapunguzia nini madaktari hao katika hadhi yao.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba swali lake Nam. 28 lenye vifungu (a), (b), na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, siyo sahihi kuwa kutokuvaa sare kunawapunguzia heshima ya kazi na kunaondoa nidhamu ya kazi. Madaktari wetu licha ya baadhi yao kutokuvaa sare au vitambulisho wanaendelea kuchapa kazi zao kwa bidii, nidhamu ya hali ya juu na kufuata maadili na sheria zote zinazoongoza kazi zao. Kutokana na hali hiyo, idadi ya wananchi wanaotumia huduma zetu za afya katika hospitali na vituo vya afya inaendelea kuongezeka siku hadi siku.

Mhe. Spika, kuvaa sare kwa madaktari na wahudumu wengine kunawaongezea haiba na ukakamavu mbele ya wagonjwa wanaowahudumia.

Mhe. Spika, suala hili la kutokuvaa sare kwa baadhi ya wafanyakazi wetu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tumeliona na tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kulitatua kwa haraka iwezekanavyo pamoja na kuwapatia vitambulisho wafanyakazi wetu wote ambao hawana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri juu ya hali halisi ya madaktari wetu, wauguzi na wengineo kwa kuvaa sare au kutokuvaa sare. Suala kubwa pahala pa kazi wafanyakazi wa

sehemu ile hutakiwa hasa wavae sare. Kwa mfano, mwanafunzi ili kumtambua kama ni mwanafunzi anasoma shule ya msingi au sekondari basi huwa na alama yake ya sare na nembo, kwa kuwa Mhe. Waziri wamesema kuwa pamoja na madaktari wetu au wauguzi kutokuvaa sare lakini kazi zinakwenda vizuri. Je, kwa watu wanaokuwa na matatizo ya kutokumtambua daktari kama yule aliyekuwa hakuvaa sare na wakati kakutwa na shida ya ghafla anataka kumuona daktari lakini hamjui, ana mpango gani wa dharura wa kutoa vitambulisho angalau kubandika nembo ili kumjua huyu daktari na huyu muuguzi.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza daktari utamjua aidha akiwa wodini au katika ofisi yake. Daktari huvaa koti na wengine huvaa tai na kitambulisho chake. Anapoingia chumba cha upasuaji daktari hubadilika na nguo za makoti huvua na wakati mwengine hutisha. *(Kicheko)*

Muuguzi huvaa nguo nyeupe, shati kama koti nyeupe na suruali nyeupe na wanawake wengine huvaa skati nzuri na huvutia. *Orderly* pia ana kitambulisho, yeye huvaa nguo za zambarau. Sasa daktari ukitaka kumfuata hospitali au kituo cha afya anakuwa na ofisi yake sio kumkuta njiani tu kwenye koridoo huyo inakuwa si daktari. Daktari inatakiwa umfuate kwenye afisi yake kwa hali ya juu na yeye anakuhudumia vizuri.

Mhe. Spika, hili tumeliona na tutalitatua haraka iwezekanavyo madaktari wetu watavaa vizuri na vitambulivyo na waweze kujulikana pahala popote watapokuwepo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Katika mwaka mmoja ambapo kwa bahati nzuri sasa hivi tunaanza na mwaka 2009, hawa ma-*nurse* hupewa sare ngapi na wizara na madaktari hupewa makoti mangapi katika mwaka ili hili kero likaondoka?

Pili kuna wafanyakazi wa aina nyingi hospitali, haoni kwamba kuna haja ya kuweka vitambulisho vyenye rangi tofauti wakavaa wale madaktari ili hospitali zetu zikaonekana kwamba zinakwenda katika utaratibu wa kinidhamu?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, hii inategemea uwezo, tukiwa na uwezo mzuri basi tutawapatia kwa kadiri inavyowezekana. Kwa sababu nguo yoyote hufuliwa, hupigwa pasi, hubadilishwa kwa hivyo lazima uwe na zaidi ya moja, mbili au tatu na madaktari wetu ni maridadi wanapendeza na wengi wao wanajinunulia wenyewe sare zao ili wazidi kuwa wazuri. Tunawapongeza madaktari wetu, wauguzi, ma-*ordarly* wote wanavaa vizuri mpaka sasa hivi tatizo hilo halipo wanapendeza kabisa.

Suala la kwamba mara ngapi hii inategemea uwezo wetu, tukiwa na uwezo tutawapatia kwa kadiri ya uwezo wetu lakini idadi ni vigumu kueleza kwa sababu inategemea uwezo wetu.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Sare sio peke yake inayomjuilisha mtu kujulikana kuwa daktari, yako mambo mengine. Hivi karibuni tulipokuwa kwenye kamati madaktari walisema hata wao wenyewe hawajuani nani daktari nani *nurse* na walimuomba Mhe. Waziri wao afanye kitu kinachoitwa *scheme of service. Scheme of Service* na *Scheme of Salary* vina tofauti lakini mimi si mtaalamu wamesema hao madaktari. Walisema *scheme of service* itapata kumjua huyu daktari, huyu *nurse*, huyu mkunga.

Kamati yetu iliombwa imshauri Mhe. Waziri ili kitu hicho kifanyike lakini Mhe. Waziri akajibu kwamba kwa sasa hali ni ngumu, lakini Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii alisema jukumu hilo atalichukua yeye na posho atawalipa wajumbe wenzangu akiwemo Mhe. Haji Faki Shaali. Je, Mhe. Waziri hili suala ambalo wameliomba madaktari umelichukulia hatua gani ili wao wenyewe kuweza kujua baada ya kuwachambulia hiyo *scheme of service*.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, hili ni suala jipya kabisa, Mhe. Mwakilishi anataka kujua habari ya *scheme of service*. Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilipotembelea wizarani kwangu ilitaka kuomba kusaidia kuharakisha mambo ya *scheme of service*, yaani wajijue mishahara yao mizuri, posho zao na mambo mengine yote. Mhe. Spika, mambo haya hivi sasa yameshaandaliwa na yako juu ya meza yangu na hivi karibuni tutachukua hatua kuiarifu Serikali Kuu kuhusu mapendekezo yote yaliyotolewa na Idara ya Utumishi Serikalini pamoja na ofisi ya Naibu Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi.

Nam. 44
Ubadilishaji wa Nambari za Vyombo vya Moto

Mhe. Hasnuu Moh'd Haji – Aliuliza:-

(a) Kuna haja gani kwa sasa hivi kubadilisha namba za magari?

(b) Na kama kuna haja kwa nini namba hizo zikawa zinabadilishwa na ajenti mmoja tu?

(c) Mhe. Waziri, huoni utaratibu huu unaleta usumbufu kwa walio na magari?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Spika awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuweza kuhudhuria katika Vikao vya Baraza ili kutekeleza majumu yetu ambayo tumepangiwa.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 lenye vifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

Serikali iliamua kubadilisha utaratibu wa usajili wa nambari za magari ili kwenda na wakati. Aidha, hatua hiyo ililenga kwenda sambamba na mfumo unaotumika katika nchi mbali mbali. Utaratibu huu pia unatumiwa na nchi zote za *SADEC* na umeonesha kuwa na mafanikio makubwa.

Utumiaji wa wakala mmoja katika ubadilishaji nambari za magari ni utaratibu wa ndani wa Bodi ya Mapato Zanzibar ambao ndio wakala wa kusajili magari. Lakini kwa mujibu wa taratibu za Bodi ya Mapato (*ZRB*) ilitangaza tenda na alieshinda tenda hiyo ndiye aliyepewa kazi ya kuandika nambari za magari. Kwa kawaida serikali huwa na utaratibu mzuri wa kutangaza zabuni kwa shughuli zake ili kupata udhibiti na ubora wa shughuli inayohitajika. Kwa mfano, pasi za kusafiria, vitambulisho vya Mzanzibari na kadhalika.

Lengo la serikali ni kutoa huduma bora ya kileo isiyo na usumbufu. Hata hivyo, kwa vile utaratibu huu ni mpya inawezekana zikajitokeza kasoro ndogo ndogo ambazo Ssrikali inaahidi itajitahidi kuzirekebisha.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Utaratibu walioufuata ni mzuri lakini unaonekana umewanyang'anya baadhi ya raia wa Zanzibar kupata zile ajira ndogo ndogo.

Kifungu cha 18(2) kinasema:

> "Kila raia ana haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matokeo mbali mbali nchini duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli zao".

Hivyo haoni kutokuwapa taarifa watu amewanyang'anya watu shughuli zao kinyemela hasa zile za kuandika andika namba na mambo mengine. Wizara yake haoni imefanya kosa kubwa kwa raia wa Zanzibar?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika jibu mama ni kwamba lengo la serikali ni kudhibiti suala zima la fedha kwa sababu kama tunavyoelewa serikali yetu inategemea

zaidi vyanzo vya mapato. Kwa hivyo, kuweka katika utaratibu huo wa taasisi moja basi ni kudhibiti hilo suala ambalo linaweza kutokezea la kukosekana kwa mapato vizuri.

Mhe. Mohammed Ali Salim: Mhe. Spika, nashukuru naomba niulize swali la nyongeza.

(a) Ni kampuni gani iliyoshinda zabuni?

(b) Je, Mhe. Naibu Waziri anaweza akatuorodheshea thamani halisi ya kutengeneza vipande vile viwili vya nambari vya kutia huku na huku kwa mujibu wa zabuni hiyo?

(c) Katika fedha inayopatikana serikali ina sehemu gani na kampuni ina sehemu gani. Je, zabuni hiyo haionekani kama kuna dalili ya harufu harufu ya rushwa?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, naomba nikazie majibu ya Mhe. Naibu Waziri wangu kwa kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mohammed Ali Salim.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kazi hii ni ya serikali na *tender* hii haikutoka Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, hii imetoka *ZRB* na kwa bahati nzuri katika mwaka wa bajeti Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Anayeshughulikia Fedha na Uchumi alilieleza hili. Kwa hivyo, pia serikali ilisema kwamba itafanya hivi na serikali imefanya.

Serikali imefanya suala hili kwa faida ya wananchi na serikali yenyewe, kwa sababu serikali imebaini kwamba kuruhusu kila mtu kuandika namba kuna mambo mengi mpaka ya ujambazi, namba nyengine zinakuwa za bandia. Lakini tumetoa tenda na Kampuni ambayo imeshinda tenda ni ya Juma Buda. Hii wameshinda kwa vigezo ambavyo wameshindanishwa na watu wengi, kila aliyetaka tenda ilitangazwa kwenye magazeti na waliotaka kushiriki walishiriki.

Sasa mimi naomba nichukue nafasi hii labda pengine kuelezea gharama halisi pengine kwa huyo anayesajili gari siwezi kuelezea faida ya serikali na kampuni. Mfano *plate number* kwa gari ni 35,850 unachangia na shilingi 750 za stika. Halafu kwa vespa ni shilingi 21,850 na pikipiki ni shilingi 27,875. *Road licence* kwa gari ambazo chini ya tani tatu, ni shilingi ishirini 24,000, lakini kuanzia tani tatu na kuendelea ni shilingi 70,000 na tani mbili ni shilingi 40,000 na tani zaidi ya kumi ni shilingi 200,000. Halafu kuna gamba la gari chini ya tani tatu na nusu ni shilingi 50,000 zaidi ya hapo ni shilingi 60,000. Vespa shilingi 25,000 na *Ciao* shilingi 10,000.

Mhe. Spika, gharama hizi kwa jumla unaziona kubwa kwa mwaka wa kwanza lakini mwaka wa pili zote zinakuwa hazipo isipokuwa inabakia *road licence*. Kwa hivyo, nafikiri wananchi wote baada ya kupata gharama kwa mwaka wa mwanzo mwaka unaofuatia mambo yanakuwa mazuri.

Lakini pia kwa gari ambazo zina usajili wa Bara zinatakiwa hapa zibadilishwe na zile zitakazoingia kutoka Bara zinapewa miezi mitatu na zitalipa U$ *30* na baada ya miezi mitatu kama anataka kuendelea na nambari za Bara alipe tena ada ile ili aendelee. Nafikiri utaratibu huu ndio ambao Waheshimiwa pia tulikuwa tukiulalamikia kwamba gari zetu zikienda zinatozwa faini. Kwa hivyo, na sisi kwa miezi mitatu ya mwanzo watalipa U$ *30*. Mhe. Spika, naomba kuelezea hayo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kwa kuwa huu mpango ni mpya na uzuri wake unajulikana ni kwa nini wale ambao wameshakata *road licence* wakalazimika kubaki mpaka kuja kukata *road licence* kwa gharama yote kubwa hiyo baada ya kufanya usajili tu peke yake.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kama tulivyosema mwanzo hili ni zoezi jipya na hatutaki kulifanya nusu nusu tunataka mambo yote yafanyike kwa pamoja umalize ili usiwe na tatizo tena kurejea *ZRB* au Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Umalize shughuli yako na mwakani ukalipe *road licence* tu mambo mengine utakuwa umemalizana nayo.

Nam. 78

Ushughulikiajii wa Mashamba ya Serikali Pemba

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza**:-**

Kwa kuwa Serikali kupitia Idara ya Ardhi na Usajili inamiliki mashamba mengi katika kisiwa cha Pemba na kuwa mashamba haya hayaeleweki vizuri.

(a) Kwa kuwa wizara haijaelewa vizuri mashamba hayo ambayo yana miti mingi ya kudumu ikiwa ni pamoja na mikarafuu, minazi, miembe, mivule na miavi, Je Mhe. Waziri huoni kuwa hali hii huisababishia hasara serikali yetu.

(b) Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa mashamba haya yanashughulikiwa ipasavyo.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 78 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, hivi sasa idara inayosimamia uendeshaji wa mashamba ya eka ni Idara ya Utawala wa Ardhi. Idara ambayo iliundwa rasmi mwaka 2006 na kupewa majukumu hayo miongoni mwa majukumu yake. Hata hivyo Mhe. Spika, idara hii pamoja na ile ya Ardhi na Usajili hazimiliki mashamba ya serikali isipokuwa zinasimamia uendeshaji na utaratibu wa ugawaji ardhi kwa matumizi mbali mbali yakiwemo matumizi ya kilimo. Mhe. Spika, wizara inayomiliki mashamba ya serikali ni Wizara ya Kilimo. Wizari hii humiliki mashamba hayo kwa ajili ya utafiti, majaribi na shughuli nyengine zihusikanazo na mambo hayo.

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba wizara haina kumbukumbu nzuri za mashamba yote ya eka tatu, hasa yale ambayo wamiliki wake wa awali wamefariki, wameyatupa au kuyakataa mashamba hayo kwa sababu mbali mbali bila kutoa taarifa serikalini. Mashamba haya huhodhiwa na watu wengine wasiostahiki bila ya wizara au idara inayohusika kuwa na taarifa rasmi. Matokeo ya baadhi ya mashamba hayo yanakuwa mabaya kwani mengine huharibiwa kinyume na taratibu. Wizara inapopata taarifa ya mashamba ya aina hii huchukua hatua ya kuyasimamia katika uendeshaji wake.

(b) Mhe. Spika, hivi sasa serikali imeanza kuchukua hatua ya kufanya uhakiki wa mashamba yote ili kujua uhalali wa wamiliki wa maeneo hayo pamoja na uhalali wa matumizi wa maeneo hayo. Matokeo kadhaa yamepatikana miongoni mwa hayo ni kugundua kuuzwa baadhi ya mashamba hayo, kukatwa viwanja nakadhalika. Wizara yangu tayari imeanza kuwachukulia hatua waliohalifu sheria za upewaji mashamba hayo, pia itaendelea na zoezi hilo katika maeneo mengine nchini mwetu. Wizara yangu pia imo katika hatua ya kuyapitia mashamba hayo tukishirikiana na Wizara ya Kilimo na hatimae mashamba hayo kwa maagizo ya serikali yatakabidhiwa Wizara ya Kilimo kwa usimamizi kama ya serikali kwa hivi sasa yalivyo.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, suala lililoulizwa linahusiana sana na Wizara ya Fedha kama nilikuwa Mjumbe mwaka juzi na suala hili linahusiana na Idara ya Mitaji ya Umma na tayari Idara hiyo ilikuwa ishafanya tathimini ya kuona itayahakiki vipi mashamba haya ya serikali kupitia Idara ya Mitaji ya Umma. Kilichoshindikana sasa ni fedha za kufanyia kazi. Nataka nimuulize

Kaimu wa Wizara ya Fedha kwa kumsaidia Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi , Nishati na Ardhi kuwa mpango ule wa kuyaenzi mashamba haya na kupitia Idara ya Mitaji ya Umma halisi hasa ikoje ili kuokoa mali ya taifa.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kama nilivyokwisha eleza serikali imeunda Idara ya Utawala wa Ardhi ambayo iliundwa mwaka 2006 kwa lengo kuu la kusimamia mustakabali wa eka tatu zilizogaiwa baada ya mapinduzi matukufu wa mwaka 1964 ili yaendelezwe na yatumike kama lengo lile lilivyo. Mara nyengine shughuli hizi huchelewa kidogo kutokana na ukosefu wa fedha, lakini kama nilivyokwishaeleza katika jibu mama ni kwamba idara husika itaendelea kushirikiana na wengine ili kuhakikisha zoezi hili linaendelea kwa harala.

Lakini lengo la serikali ni kwamba maeneo hayo yatumike kwa ajili ya kilimo na tumeagizwa tushirikiane na Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mazingira ili sasa maeneo haya yote ikabidhiwe wizara hiyo ili ipate kuwapa wananchi kuendeleza kilimo na pia kwa shughuli nyengine ambazo zinahitaji kukuza kilimo ndani ya nchi yetu.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kuwa Idara ya Utawala wa Ardhi haimiliki mashamba lakini ni Wizara ya Kilimo, jambo ambalo wengi linatukanganya. Sasa mimi napenda niulize tatizo ambalo limejitokeza katika jimbo la Mhe. Mohamed Ali Salim hivi karibuni.

Kuna Sheha mmoja katika mji wa Mkoani alikwenda kulaghai watu wa Idara ya Upimaji wakaenda kumpimia mfanyabiashara mmoja kiwanja katika shamba la watu. Je, sasa tatizo hili hapa ndipo pa kulalamikia ni wizara yako au wizara ya Kilimo.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, Ardhi kwa mujibu wa sheria ya nchi yetu inasimamiwa na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kama ndio wanaosimamia utaratibu na matumizi ya ardhi. Mashamba ya serikali yako mashamba ya serikali na hivi sasa hili tunalolizungumzia hizi eka pengine watu wamezitupa, wameziacha ambazo hazipo kwenye utaratibu mzuri.

Kwa vile nchi yetu imedhamiria kukuza kilimo hayo yalikabidhiwa rasmi Wizara ya Kilimo mashamba ya serikali ambayo yote yanajulikana hayajakabidhiwa mwananchi mmoja mmoja, hayo yanasimimiwa moja kwa moja na Wizara ya Kilimo.

Suali la Sheha kuagiza wapimaji kupima ndani ya eneo la mtu ni jambo la kushangaza. Kwa maana eneo kapewa mtu kwa mujibu wa sheria za nchi

hawezi kujitokeza mtu mwengine yeyote hata huyo Waziri wa Wizara yenyewe ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kumuagiza mtu kumpimia mtu eneo lake bila ya ridhaa yake mtu huyo, ikiwa linahitajika na serikali kuna utaratibu wake, aidha kupitisha miradi ya maendeleo ambayo lazima wananchi wanashiriki au kwa shughuli maalum ya serikali, kuna utaratibu wake wa kwenda. Lakini hakuna mtu mwenye haki ya kumuagiza mtu kupima eneo la mtu bila ya ridhaa ya huyo aliyepewa kwa mujibu wa sheria za nchi na serikali pia ina utaratibu inaukubali.

Nam. 21

Uwekaji wa "*Tours*" Ndani ya Hoteli za Kitalii

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza**:-**

Hivi sasa kuna malalamiko kutoka kwa wananchi dhidi ya baadhi ya wamiliki wa hoteli za kitalii kutokana na kuweka ofisi za kuratibu utembezaji wa wageni *tours* ndani ya hoteli hizo, kinyume na kazi hii kufanywa na wananchi wetu ili kuongeza ajira na kuwapunguzia umaskini.

(a) Mhe. Waziri, je kitendo cha wenye mahoteli kutembeza wageni kwa kutumia ofisi za kuratibu utembezaji wa wageni (*tours)* zilizomo ndani ya mahoteli yao, kinakubalika kisheria.

(b) Je, huoni kuwa ni busara kwa ruhusa hii ikatolewa kwa wananchi wetu wazalendo ili kuinua hali zao za kimaisha.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 21 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wenye mahoteli kisheria hawaruhusiwi kufanyakazi ya kutembeza watalii. Wanachoruhusiwa ni kuhamisha watalii kutoka sehemu za kuingia nchini kama *Airport* na bandarini na kwenda hotelini kwao. Sheria ya Utalii ya mwaka 1996 imetoa fursa kwa Wazanzibari tu kufanya kazi hiyo. Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna malalamiko na hasa kutoka kwa *ZATO* kwamba mahoteli yamekuwa yakifanya kazi hiyo.

Mhe. Spika, tumegundua pia kwamba kuna kampuni za wazalendo walioajiri wageni kuwafanyia kazi hiyo na sura hiyo nayo pia inatoa taswira kwamba wageni wanafanya kazi ya kutembeza wageni. Hata hivyo Kamisheni ya Utalii pamoja na *ZATO* wanalifanyia kazi suala hili ili liendeshwe kisheria.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwamba kakiri kwamba hili suala lipo na kero kwa wananchi wetu. Lakini mtalii Mhe. Spika, anapoingia katika nchi na anapokuwa huru wa kumtembea sehemu anayotaka bila ya bughuza huwa anaitangaza ile nchi vizuri na akirudi kwao huwa analeta wageni zaidi kwa taarifa nzuri ya kutokuwepo usumbufu katika nchi.

Kwa kuwa hivi sasa baadhi ya watalii huchukuliwa kutoka Nungwi na kwa kuwa wale wenye mahoteli mpango huu unakwenda siri au dhahiri katika maeneo yao. Kwa kuwa mtalii yule kachukua gari nje ya zile *tours* zilioko ndani ya mahoteli yao wakifika longa longa huzuiliwa inapigwa simu warudishwe wanakotoka kwa sababu ile gari waliochukua siyo, au mfano wanapofika Mahonda au Mfenesini hutokea kwa kutumia baadhi ya polisi kwa ujanja wa kushirikiana na wenye mahoteli ili kuleta bughuza kwa watalii. Je, Mhe. Waziri hili analitolea wito gani kwa hawa watu wa usalama barabarani (polisi) na hawa wanaoweka vituo vya utalii ili kutokuwabughuzi watalii ili wakirudi kwao waitangaze nchi yetu vizuri.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, Mhe. Ali Suleiman Ali ameshaliuliza kabisa swali ambalo angeniuliza kesho ambalo ninalo kwenye *list* na majibu yake ni kwamba naomba nikubaliane naye kwamba hayo yanatokea na kwa sababu ya usumbufu huo na malalamiko tuliyoyapata tarehe 18 Januari tulipokuwa na mkutano wa *Zanzibar Tours Operators*. Kamisheni ya Utalii pamoja na *ZATO* wanalifanyia kazi hili, kuna aina mbili za kurejesha wageni njiani. Aina moja ni kweli kwamba mahoteli wanatumia polisi kurejesha wageni wanapochukuliwa na *tours operators*.

Lakini aina ya pili kwamba Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wanawarudisha wageni wanaofanyiwa *tour operation* na mahoteli. Kwa hivyo, inaweza si mahoteli na polisi lakini Kamisheni ya Utalii pia na Polisi ili kurekebisha hali. Nasema tatizo hilo lipo na tunalifanyia kazi ipasavyo na matumaini yangu Mhe.Spika, kesho Mhe. Ali Suleiman swali lake atalifuta. *(Makofi/ Vicheko).*

Nam. 9

Tatizo la Kuingia Maji ya Bahari katika Mashamba ya Kilimo

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza**:-**

Kisiwa Panza na visiwa vyengine vidogo vidogo vilivyo karibu na bahari Pemba, vimekuwa vikikabiliwa na tatizo la kuingia kwa maji ya bahari na kuathiri mashamba ya kilimo cha wakulima wa visiwa hivyo, na kama tatizo

hili halitashughulikiwa ipasavyo, kuna hatari ya maji hayo kufika viamboni na kuleta athari kubwa zaidi. Kwa kuwa tatizo hili ni kubwa. Je, serikali imeshachukua hatua zipi za kulikabili
tatizo hili?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira – Alijibu**:-**

Mhe. ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba maeneo mengi ya kilimo ya Kisiwa Panza pamoja na maeneo mengine Unguja na Pemba yameathirika kwa kuvamiwa na maji ya bahari. Hii inatokana na matatizo ya kupanda kwa kina cha bahari ulimwenguni sambamba na harakati za kimaisha za wananchi hasa ukataji wa mikoko, kuchukua mchanga wa pwani kwa shughuli za ujenzi pamoja na kuvunja matumbawe.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na matatizo haya na hasa Kisiwa Panza, serikali ilikwisha watuma wataalamu wake kufanya tathmini ya kina juu ya njia za kuchukuliwa ili kuondosha tatizo hilo. Tathmini hiyo imeshakamilika na imetoa mapendekezo juu ya hatua za kuchukuliwa. Maeneo yaliyofanyiwa tathmini hiyo ni pamoja na Mto wa Kae, Tunguu na kwa Moleni. Hivi sasa tunaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga kingo kuzuia maji hayo.

Aidha, napenda kutoa wito kwa wananchi wa maeneo yote kuwa tuzitunze raslimali zetu hasa za pwani ikiwa ni pamoja na kutochukua mchanga wa pwani kwa matumizi yoyote ili tuepukane na matatizo mbali mbali kama vile kupanda kwa maji ya bahari katika majenzi na maeneo ya kilimo. Ahsnate sana.

Mhe. Omar Ali Jadi: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri kakubali kuwa matatizo haya yanatokea sehemu mbali mbali na kataja eneo la Kisiwa Panza kwamba serikali imeshaleta wataalamu wake kwenda kufanya utafiti na serikali tayari imeshapeleka wataalamu wake katika kisiwa cha Unguja na Pemba. Je, serikali inayo habari kama kijiji cha Shengejuu kwamba kuna maeneo yameshavamiwa na maji chumvi na kama mna habari kwa nini katika orodha yake asiitaje?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, pale niliposema na maeneo mengineyo nilikuwa na maana yale maeneo ambayo sikuyataja nilifupisha tu pale. Lakini sio Shengejuu peke yake hata lile eneo ambalo nililotoka mimi Micheweni nalo linafanyiwa tathmini na limo katika kuvamiwa na maji ya bahari na mashamba ya kilimo yanaathirika.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, kwanza ningependa kujua licha ya haya maeneo yanayonihusu katika jimbo langu la Kisiwa Panza. Lakini pia kinchi maana yake mimi nilikutana na ujumbe mkubwa bahati mbaya sikwenda, wataalimu wa *World Bank* tukaambia kuwa Waheshimiwa tunafuatilia hili tatizo lako si la peke yako.

Kwanza, sasa kama si peke yangu hizo tafiti zimefanyika maeneo gani mengine katika visiwa vya Unguja na Pemba kubaini hali kama hii ya uharibifu wa mazingira haya.

Pili, kwa taarifa tulizonazo kuna wakati ilikuwa fedha tayari zimeshapatikana na hata wananchi wameshaarifiwa kuwa tayari zimeshapatikana, lakini kwa ghafla kwa mshangao zile pesa naona hazikufika mpaka leo sijui fedha hizi zitafika lini.

Tatu, Mhe. Spika, wakati alipokuwa Mhe. Kamali Basha waziri wa wizara hii kwa kushirikiana na mimi tulikwenda na tukasaidia sehemu moja hivi, tukasaidia pamoja na Mbunge tukaondoa tatizo hili lakini sehemu ile bahati nzuri kaiweza sasa imetiribua sehemu nyengine ambayo inaathiri sana maeneo ya wananchi.

Mhe. Spika, je, ikiwa tutachelewa kwa muda mrefu na sasa hivi maeneo mengi ya Kisiwa Panza yalikuwa yameshaharibika hatuoni kwamba wananchi watashidwa kulima.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwa kweli tunajitahidi na tulivyosema mbali ya kufanya ile tathmini moja katika kazi nyengine ya ziada ni kuomba wafadhili watusaidie ili tuweze kukamilisha kazi yetu kubwa. Serikali iko mbioni kufanya kazi hiyo na serikali yetu pia itafanya kila jitihada pale ambapo kutakuwa na uwezekano basi itaweza kulifanyia kazi.

Miongoni mwa maeneo tulikuwa tumetaja Kisiwa Panza mengine tulikuwa tumeacha, lipo eneo kama hilo la Kilimali ambalo pia limevamiwa na bahari na tumeshalifanyia tathmini na maeneo mengine yale ya Pemba wataalamu wetu wanaendelea kuyazunguka siku hadi siku. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, kwa kuwa kisiwa hiki matatizo ya kupindukia maji ya chumvi si mara moja wala mbili na kwa kuwa kisiwa hiki kina watu wengi ambao mazao yao yameharibiwa na maji chumvi. Licha ya Kamati ya Fedha na Uchumi kufanya ziara kuona hali hiyo. Je, Mhe. Spika, ni lini wizara yake ikishirikiana na Wizara ya Maji itafanya ziara kukitembelea

kisiwa hicho pamoja na kuwaona wananchi athari ya maji chumvi kupindukia juu na athari za mazao yao kuharibika kwa mazao ya wananchi.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, nataka kuongezea jawabu za Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo kama Kaimu Waziri wa Kilimo.

Mhe. Spika, Idara ya Mazingira pamoja na Kamisheni ya Utalii pamoja na watu wa Ardhi walifanya zaira Unguja na Pemba katika vijiji mbali mbali, kwa Unguja walikwenda Michamvi, walikwenda Kaskazini Nungwi, Kiwengwa na kwa Pemba walikwenda sehemu zote nne na katika ziara zile yaliogundulika ni kwamba ni kweli maji ya chumvi yanaingia kwenye mazao ya wananchi na sababu kubwa ni ukataji wa mikoko na kuna ripoti ya serikali imeandikwa ambayo hata Mhe. Waziri Kiongozi anajua na katika moja ya zaira zake Pemba aliwaasa wananchi katika ukataji wa mikoko. Kwa sababu mikoko ndio inayozuia maji ya chumvi yasifike kwenye mashamba. Lakini kwa bahati mbaya wananchi wanakata mikoko na kwa bahati mbaya katika kijiji kile lugha ya mikoko haikuwa ni lugha nzuri kwa hiyo alipata jawabu ya kushtuza kidogo.

Lakini ninachotaka kusema ni kwamba tatizo linajulikana na serikali na sasa hivi tuko Idara ya Mazingira na sekta nyengine kama Utalii na Ardhi tunalifanyia kazi suala hilo vizuri.

SHUGHULI ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na mambo mengine yanayohusiana na hayo
(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi nikaweza kuchangia kidogo tu kwenye mswada huu wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia.

Kwanza niombe radhi kwa mujibu wa hali yangu mkiona nimenyamaza niacheni nipumzike.

Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uwezo leo kuja hapa na kunipa nafasi nikaweza kuchangia huu mswada.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Elimu. Hili ni jambo kubwa na zuri kwa upande wetu wananchi wa Zanzibar na mtu ukimuona kama hivi ujue ana kitu cha kufikiri. Zanzibar tuna matatizo ya somo ya sayansi maskulini na tuna matatizo ya walimu wa sayansi.

Lakini kufikiri hili akaweza kulileta na jambo la busara sana. Mhe. Spika, mwanzo wa ngoma ni lele hatuwezi kupiga ngoma kwanza kabla ya vigelegele. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Elimu ameaanza kupiga vigelegele na Mwenyezi Mungu atamsaidia aliweze hili jambo na kama hakuliweza atakuwa amelianza na atakayekuja yeyote ataliendeleza kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kwanza mimi nilikuwa nataka nitoe ushauri kwa sababu sina maneno mengi, mambo yangu mawili matatu tu ya kutoa ushauri. Mimi ningelimuomba Mhe. Waziri wa Elimu kwamba sasa hivi tuendeleze somo la sayansi, yeye huku anafanya matayarisho ya Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Lakini tuliendeleze somo la Sayansi sana kwa sababu maskulini Sayansi inasomeshwa kama haisomeshwi. Tuna tatizo kubwa siku zote tunasema hapa linaelezewa la walimu kidogo. Lakini kitakapokuja hiki chuo walimu watapata nafasi pia ya kusoma Sayansi.

Sasa hivi kwanza tuwatayarishe wanafunzi wetu kwa ajili ya Sayansi. Sisi hapa Zanzibar A*l-hamdullilah* Mwenyezi Mungu katujaali tuna watu wenye akili au wanaopenda kusoma, kama sasa hivi watoto wetu wanasoma vizuri na toka zamani wanafunzi wazuri na walimu wazuri wanatoka Zanzibar. Kwa hivyo, naamini kwamba hili somo la sayansi kama litasomeshwa kweli kweli kuanzia chini yaani msingi mpaka sekondari, hii taasisi haina taabu itapata wataalamu.

Kwa hivyo, mimi ningemshauri Mhe. Waziri wa Elimu akaanzisha kama alivyosema sayansi na teknolojia, tungeanza na teknolojia sayansi tukaianzia chini kwanza kuisomesha, ikasomesheka. Tunataka vyote hivi sisi viwepo, lakini kwa sababu sayansi ni ndogo sana katika Zanzibar, basi isomeshwe sayansi. Tujitahidi kutafuta walimu wa sayansi hata kama ni kwa gharama, ili watoto wetu wapate kusoma sayansi waelewe vizuri, na halafu tunapofungua taasisi yetu tusiwe tena tunahangaika kutafuta wanafunzi. Wanafunzi wawe tayari wameshatayarishwa.

Mhe. Spika, hiyo taasisi si kama inasemwa leo na kesho inaanzishwa hapana. Ina maandalizi yake. Namwomba Mhe. Waziri kwa hisani yake ajitahidi kutafuta kwanza nyenzo, asije akaanzisha taasisi kabla ya nyenzo kuwa nazo mfukoni, na awe na mfuko wa kufanyia hiyo kazi. Ikiwa mfuko hakuna, basi bora asianzishe kwanza. Atafute mfuko wa kusomeshea watu sayansi mpaka wawe wameelewa, halafu ndio aanzishe taasisi. Lakini kama atakuwa na mfuko maalum, basi aanzishe chuo, maana sasa hivi tuko kwenye sayansi na teknolojia ndio karne yetu hii. Kwa hivyo, ni vizuri na sisi tusiwe kila siku wa mwisho. Maana mambo mengi sisi ni wa mwisho hapa. Hata wenzetu Bara wanatuoneaonea kwa sababu sisi ni wa mwisho.

Mhe. Spika, mimi ningeshauri kitu kingine. Mhe. Waziri kama alivyokaa na watu wake wakavunja kichwa wakafanya hili. Kwa hivyo, waliendeleze ambapo sisi Wazanzibari tunalihitaji sana. Tunahitaji na watoto wetu wanahitaji kusomeshwa sayansi na hizo teknolojia, halafu baadae ndio tufunguwe chuo.

Mhe. Spika, sitaki kusema sana. Mhe. Spika, kuna ukurasa wa 223

Mhe. Spika: Ukiona unataka kukaa, basi nakuruhusu ukae na useme.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Mhe. Spika, katika ukurasa wa 223 kifungu nambari 9(5) kuna kitu

Kifungu cha 9(5)

> "Uteuzi wa mjumbe ambaye ameshindwa kuhudhuria mikutano mitatu mfululizo ya Baraza bila ya kuwa na sababu za msingi, unaweza kufutwa na waziri au mtu mwengine mwenye mamlaka ya kufanya uteuzi kwa ushauri wa Baraza".

Mhe. Spika, mimi nafikiri ingekuwa jambo la busara angetuwekea wazi, baada ya huyu waziri atakuwa mtu gani tena mwengine ambaye anaweza kufuta huu uteuzi, tungepata kujua vizuri zaidi.

Mhe. Spika, unajua hii Baraza na bodi hili jambo lilitokea katika Wizara ya Habari, na nilishauri pia Wizara ya Habari kwenye Baraza nafikiri la Sanaa kama sitokosea. Baraza bodi ni vitu viwili ambavyo vinachukua nafasi kubwa sana kwenye kazi. Lakini kwa nini kisifanywe kitu kimoja kikawa kitasaidia kwa vyovyote kupunguza gharama.

Baraza lilichaguliwa Mwenyekiti na Rais, lakini humu kidogo nimeona tofauti na ilivyokuwa kwenye Baraza la Sanaa na bodi yake. Huku Mwenyekiti anakua yule Mkurugenzi ambaye yuko kwenye Baraza, ni jambo la msingi. Lakini kwa kuona gharama zitakuwa nyingi, kwa nini kisifanywe kitu kimoja ambacho kinaweza kufanyakazi kwa zote mbili. Nafikiri Mhe. Spika, nimechangia kidogo.

Mhe. Spika: Ahsante sana, pole sana Mhe. Aziza na hali yako hiyo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi asubuhi hii kutoa mawazo yangu katika mswada huu uliowasilishwa siku ya Ijumaa, ambapo na mimi nilikuwa kwenye semina, lakini sikupata kuuchangia. Kwa hivyo, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na ninaomba univumilie kama

itakuwa wenzangu tayari wameshayazungumza nitakayosema mimi, basi na mimi nilikuwa nimelenga niyaseme kwa nia nzuri ya kuboresha mswada wetu.

Kwanza namshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa kuleta mswada huu ambao unakigeuza Chuo chetu kilichokuwa cha Ufundi Karume, na sasa kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia. Nadhani hili ni jambo zuri kama walivyosema wenzangu, na sisi kwa kuwa tuko kwenye dunia, basi lazima tuwe tunakwenda na wakati tusiachwe nyuma sana. Nia ni nzuri na sababu ni nzuri, kwa hivyo hivi sasa ni kushirikiana katika utekelezaji wake.

Mimi kabla sijenda sana kwenye vifungu vitatu au vinne vya mswada, nilikuwa naomba nitowe maoni yangu juu ya kuanzishwa kwa taasisi hii. Nina mambo matatu ambayo namwomba waziri kama yatakuwa ni ya msingi, basi ayachukuwe na wataalamu wake wayafanyie kazi.

Mhe. Spika, jambo lolote lile linalotaka kuanzishwa huangaliwa sana msingi. Hata ukitaka kujenga nyumba ya ghorofa, basi msingi wake ni tofauti na nyumba ya kawaida. Kwa sababu nyumba ya ghorofa inachukua vitu vingi kuliko nyumba ya kawaida. Sasa ningeshauri na mimi kwamba tayari wizara imeanzisha taasisi nyingi kubwa kama vyuo vikuu, lakini uanzishwaji wetu huo, unakuwa tunaridhi na majengo katika kuanzisha. Kwa waliobahatika kusoma kwenye vyuo vya wenzetu, basi utakuta kinaandaliwa chuo rasmi katika mitaala yote, yaani lile jengo linachukua na mitaala ya kile chuo chenyewe. Kwa hivyo, kwa vile na sisi ndio tunaanza, basi si vibaya tukaanza hivyo.

Mhe. Spika, nilikuwa nashauri vile vile chuo tukikitangaza na kwa kuwa ni kitu cha maendeleo katika dunia, nadhani tutapata wenyeji kutoka nchi mbali mbali kuja kujiunga kwenye chuo chetu. Kwa hivyo, ningeomba kitu cha kwanza Mhe. Waziri tukishapitisha sheria hii, basi na chuo chetu cha Karume tungekibadilisha kidogo, kwa sababu ni chuo cha zamani, majengo mengi sasa hivi yameanza kuzeeka. Kwa hivyo, tungepiga sopu sopu kidogo, angalau wakija na wenzetu kujiunga katika chuo wakajua ndio hiki ni chuo

Sasa nilikuwa namwomba Mhe. Waziri kama hilo ataliona ni la busara, basi muombe mfuko pahala muanze kukarabati au kutengeneza majengo yetu, hasa sehemu ya daghalia na sehemu ya madarasa.

Lakini jambo la msingi chuo kinahitaji walimu, na walimu sasa hivi ni kitu ghali sana, hasa walimu wa elimu ya juu. Kwa sababu wenzetu wanatangaza biashara hiyo na mtu kama ana sifa anakwenda anajiunga. Kwa hivyo, kama hatukuandaa mazingira mazuri, basi pengine hao hao tutakaowaanzia chuo na wao watatukimbia. Kwa hivyo, ningeomba nyumba za Karume za walimu

haziko katika hali nzuri, naomba na hilo litizamwe, na mitaala mingine kama itakuwa wataalamu ndani ya nchi yetu hakuna, basi tunaweza tukaagiza mtaalamu nje akaja, na akifika angeridhika akishaona hali ya maandalizi yetu katika uanzishwaji wa chuo hicho. Sasa naomba na hili waziri kama litakuwa ni la busara, basi wewe na wataalamu wako mlifanyie kazi hiyo, ili kila mwenye haja ya kuja pale, basi akija aridhike.

La tatu Mhe. Spika, katika mchango wangu juu ya mswada huu ni kuhusu maslahi ya wale ambao wataifanya kazi hiyo. Hivi sasa nadhani maslahi yapo, lakini kwa kuwa tunatoka ngazi moja tunaunda ngazi nyengine, basi na maslahi yangetengenezwa kwa vizuri, ili yeyote yule anayetaka kuja pale kutoa mchango katika kuelimisha wanafunzi wetu maslahi yasimzuwie, yamvute ili aweze kutusaidia katika kukiendeleza chuo chetu. Nadhani katika mambo yangu hayo matatu ya mwanzo kabla sijaugusa mswada, Mhe. Waziri pamoja na wataalamu wako kama yatakuwa ni ya msingi, basi naomba muyachukue na kuyafanyia kazi.

Sasa Mhe. Spika, nakuja kwenye Mswada wetu katika ukurasa wa 226, hapa pana kifungu cha 21 ambacho kimezungumzia juu ya suala la "rufaa". Kwa hivyo, kifungu cha 21 kuna (1),(2),(3),(4) na (5). Nitaanza na kifungu cha 21(4) ili nipate mtiririko mzuri. Kinasema kwamba;

Kifungu cha 21(4)

"Katika kusikiliza rufaa chini ya kifungu hiki, Baraza linaweza";

(a) Kuweka pembeni uamuzi utakaotolewa dhidi ya mwanafunzi au mfanyakazi na adhabu iliyotolewa dhidi yake au

(b) Kukubaliana na maamuzi pamoja na adhabu au

(c) Kukubaliana na maamuzi na kupunguza au kuongeza
adhabu iliyotolewa dhidi ya mwanafunzi au mfanyakazi.

Sasa hoja yangu iko katika nambari (5) inasema;

Kifungu cha 21(5)

"Uamuzi wa Baraza chini ya kifungu hiki utakuwa wa mwisho".

Mimi nilikuwa nina mawazo juu ya sentensi hii, kwa sababu hivi karibuni wenzetu Chuo Kikuu walikuwa wana mzozo mkubwa wa wanafunzi juu ya kudai haki ya misaada inayotolewa na serikali katika usomeshaji, ulikuwa hauwapi tija wale wanafunzi wenye kipato cha chini. Kutokana na hali hiyo baada ya mzozo kuwa mkubwa watu wamekwenda Mahakamani.

Je, na sisi kama tutaacha uamuzi wa mwisho uwe ni wa bodi. Je, mtu akienda Mahakamani masuala haya yatakwendaje. Nilitaka Mhe. Waziri anipe ufafanuzi, kwa sababu hivi sasa vyombo vipo vya utawala bora, mtu hakuridhika na uamuzi wa taasisi anakwenda Mahakamani kwa ajili ya kufungua mashtaka na kudai haki zaidi.

Je, likitokezea kama hili, kisheria tutaweza kujitetea vipi au litahifadhi vipi suala hili. Nadhani kwa nilivyokusudia Mhe. Waziri kanisikia na anaweza akanipa maelezo ya ziada atakapokuja kufanya majumuisho.

Mhe. Spika, nikiendelea kifungu cha chini yake hapo, yaani kifungu cha 22, kinasema "kubakiza". Naomba kunukuu.

Kifungu cha 22

> "Tendo lolote halali lililofanywa na Chuo cha Ufundi cha Karume kabla ya kuanza kutumika kwa sheria hii litakuwa halali kama limefanywa chini ya masharti ya sheria hii".

Mhe.Spika, yaani kifungu hiki kinasema jambo lolote la chuo ambalo hivi sasa lipo katika mpango pengine, kwa hivyo likianzishwa suala hili litakuwa halali katika utekelezaji wake, yaani imekusudia kama italichukua, basi itachukuliwa kwenye sheria hii ya chuo kipya kinachoanzishwa, ili kuweza kutekelezwa jambo la halali.

Sasa nina wasi wasi kwamba yapo mengine utayaona kama si halali, lakini pia ni halali.

Kwa mfano, kama wana kesi za wanafunzi pengine wamefukuzwa na wako Mahakamani, hili utaona kama si halali, lakini upande mmoja lina uhalali. Je, ikitokezea kama hivyo, chuo wakati wa kubadilisha kuna matatizo kama haya. Je, na haya yatakwenda kwenye sheria mpya au yataachwa tu yamalizike. Nilikuwa naomba na hilo nipatiwe ufafanuzi.

Mhe. Spika, nikija kwenye ukurasa wa 224, hapa panazungumziwa Sehemu ya Nne, Masharti ya Fedha. "Fedha za Taasisi". Mhe. Spika, naomba ninukuu kidogo.

Kifungu cha 14

" Fedha na mapato ya taasisi yatakuwa:
14(a) Fedha zile ambazo zitatolewa na serikali kwa ajili ya taasisi".

Halafu kuna (b),(c),(d) na (e). Hoja yangu iko kwenye (a) na (e). Sasa naona bora nisome kabisa halafu ndio niseme kwa pamoja. Kijifungu kidogo cha (e) kinasema:

Kifungu cha 14(e)

"Ada za taasisi na malipo mengine yanayotokana na huduma zinazotolewa na taasisi".

Mhe. Spika, nitaanza hii ya chini. Najua kwamba vyuo vingi vinakuwa na ada yake kwa mwanafunzi pengine wa *private*, ama mwanafunzi ambaye katoka kwenye mitaala na kaingia pale kwa sifa zake pengine za mitihani kama utaratibu wa serikali unavyoeleza. Lakini patakuwa na ada na ada hizo zitakuwa kwenye mapato ya taasisi yenyewe.

Suala langu liko hivi. Hivi sasa vyuo vingi vimeanzishwa hapa kwetu, lakini utakuta wanafunzi wengi wanahangaika kusoma kwa sababu zile ada zake zinakuwa kubwa. Je, Mhe. Waziri na hili pia mmelitizama katika mswada huu ambao tunaanzisha taasisi yetu mpya, kwamba wananchi wengi na wanafunzi wengi wa nchini kwetu hapa ni maskini. Kwa hivyo, naomba na hili litizamwe, tusianzishe taasisi ikawanufaisha sana watu wa nje kuliko sisi wenyewe, itakuwa "punda wetu wenyewe halafu tunakaa mkiani".

Kwa hivyo, naomba hili litizamwe, ili ile tija iliyokusudiwa iweze kupatikana juu ya ada ili wanafunzi waweze kusoma. Kama watalala chuoni au watakwenda na kurudi, lakini ile ada inayowekwa basi ikidhi haja na matakwa ya nchi yetu, kwa sababu tukiongeza kidogo kutokana na hali zetu, kwa sababu sasa hivi elimu pia tunaichangia, daftari ununuwe, kalamu ununue, usafiri wa kukupeleka ulipe na masomo ulipe. Kwa hivyo, naomba na hili tulitizame ili lile lengo tulilokusudia na dhamira ziweze kufanikiwa na tupate wataalamu wetu kutoka katika nchi yetu.

Lakini kifungu cha 14(a) kinasema; "fedha zile ambazo zitatolewa na serikali kwa ajili ya taasisi", nadhani hii ni ruzuku. Hili pia ni suala muhimu, taasisi nyingi sasa hivi serikali ikichelewa kutia fedha panaingia misukosuko mingi. Kwa hivyo, naomba hii sheria hili suala kama wizara ilisimamie vizuri na serikali inasikia kwamba tukianzisha na kwa kuwa ni kitu kipya, basi ruzuku lazima iende kwa wakati ili yaweze kwenda mambo yetu kama tulivyoyapanga. Kama tutaanzisha, halafu ruzuku ianze kuchelewa kwenda, basi itaonesha

kwamba hata ule utekelezaji wa kazi yetu utapungua kasi tuliyokusudia. Serikali ipo, inasikia na wizara inasikia. Kwa kuwa kitu tunakianza, basi lazima ruzuku ifike mwanzo ili waweze kupanga mipango yao, na hizi ada za wanafunzi waongezee katika mapato ya kuendeshea taasisi yetu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika ukurasa wa 221, huu ni mchango wangu wa mwisho, kwa sababu mswada ni mfupi na nimetoa maoni yangu na pia kwenye mswada nimetoa maelezo mle ambamo sikufahamu, basi nifahamishwe. Hapa kwenye Sehemu ya Tatu inasema kwamba Utawala wa Taasisi, kutakuwa na Baraza. Mwenzangu amezungumza aliyeondoka sasa hivi kwamba kuna Baraza na bodi ya wataalamu.

Sasa nadhani mimi kwa kuwa chuo chetu ndio kwanza tunaanza tungefanya moja, tungechukua bodi ama tungechukua Baraza, ili kupunguza gharama. Lakini katika Baraza nilikuwa pia nina mchango ambao naomba ninukuu; katika kifungu 6(1).

Kifungu cha 6(1)

"Kutakuwa na Baraza la Taasisi, ambalo litakuwa na wajumbe wafuatao;

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais,

(b) Mkurugenzi ambaye atakuwa mjumbe kwa wadhifa wake na atakuwa Katibu wa Baraza.

(c) Wajumbe wengine watano watakaochaguliwa na waziri, baada ya kufanya mashauriano na vyuo husika, kama ifuatavyo;

(i) Mjumbe kutoka Mamlaka ya Ufundi Stadi ya Zanzibar,

(ii) Mjumbe kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, huyo ni mjumbe wa pili huyo kama ndivyo nilivyofahamu au kama sivyo, basi Mhe. Waziri ataniweka vizuri.

(iii) Mjumbe kutoka Wizara inayohusika na elimu,

(iv) Mjumbe kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara na

(v) Mwakilishi kutoka Jumuiya ya Waajiri. Hapo inakuwa waziri nafasi zake tano zimeshatimia. Lakini kuna nambari (viii) inayosema kwamba:-

"(viii) Mjumbe mmoja atakaechaguliwa na waziri ambaye atakuwa na uzoefu katika mambo ya elimu".

Mhe. Spika, sasa inaonesha waziri hatokuwa na wajumbe watano, watakuwa sita sasa. Kwa hivyo, naona hii bora ingechanganywa moja kwa moja tu ikasema kwamba "waziri atakuwa ana nafasi sita katika kuchagua wajumbe wa bodi, na ile nambari sita ikaongezwa kwenye tano. Huku juu kaambiwa tano, halafu mwisho inaongezwa sita. Kwa hivyo, nadhani ni uandikaji tu, kama itaweza kupangwa vizuri, basi isemwe waziri ana nafasi sita na katika hizo tano na hii ya sita itaongezwa pale.

Mhe. Spika, lakini pana nafasi mbili hapa, nilikuwa nimuulize Mhe. Waziri sijui hizi atateua nani kwa sababu pana nambari (vi) ambayo inasema kwamba

(vi) Mwakilishi wa Jumuiya ya Wanafunzi ya Taasisi na

(vii) Mwakilishi wa Wanataaluma wa Taasisi

Mhe. Spika, sasa sijui hawa wanaingia kwa vyeo tu ama pia itakuwa kuna mtu anawateuwa. Ilikuwa mheshimiwa huo ndio wasi wasi wangu na nilitaka nipate maelezo kama nimefahamu ndivyo ama sivyo, basi unifahamishe.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini, tunaunga mkono mswada huu nashukuru.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata fursa ya kuweza kutoa maoni yangu kuhusiana na mswada huu wa Kuanzisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia.

Mhe. Spika, mimi katika mchango wangu kwa sababu yameshasemwa mengi, sitataka niyarudie. Kwa hivyo, nitaepuka ile kwenda kwenye vifungu vya mswada, lakini nitajaribu kutoa maoni yangu kwa jumla na huenda pengine labda mengine hayajaguswa guswa na mengine yameshaguswa, lakini nitajitahidi.

Mhe. Spika, katika mswada huu kwa mujibu wa mtazamo wangu wa kuanzishwa taasisi hii, kwanza nilikuwa naona kama ambavyo ulimwengu huu unavyokwenda wa sayansi na teknolojia, basi na sisi Zanzibar tukiwa ni miongoni mwa watu ambao tumo katika dunia hii hatuna budi kwenda pamoja na wenzetu.

Lakini pamoja na suala hilo bado Mhe. Spika, tunahitaji kujiangalia tukoje na tuna uwezo gani katika kuanzisha masuala mbali mbali yanayohusiana na mambo ya sayansi na teknolojia.

Mhe. Spika, nikianza mchango wangu nataka nianze kwenye jina la chuo. Jina la chuo linasemwa kwamba itakuwa ni Taasisi ya Sayansi na Teknolojia. Kwa hivyo, mimi niungane na wenzangu waliosema kwamba "safari ni hatua" na "mwanzo wa hesabu ni moja". Kwa hivyo, mtazamo wangu na mimi nilikuwa naona hiki chuo tusiende moja kwa moja kuingia sayansi na teknolojia kwa pamoja. Lakini tuanzie teknolojia ambayo kwa kiasi fulani ina unafuu kuliko kuichanganya na sayansi kwa sasa hivi na hili lifuatie baadae. Kwa nini nikasema hivyo Mhe. Spika, ushahidi upo.

Kwanza ni uwezo wa serikali yenyewe katika kuanzisha masuala haya ya kisayansi, jambo ambalo linahitaji gharama kubwa kutokana na vifaa. Katika kuanzisha taasisi hii hatuwezi tu moja kwa moja tukatoka na kwenda kuanzisha kitu kikubwa na cha kisasa kama hiki, kwenye majengo ambayo kwa kweli yatakuwa hayaendani na hali halisi ya hii taasisi kama ilivyo. Kwa hivyo, tunahitaji kuwa na majengo yanayofanana na taasisi yenyewe. Lakini sio majengo tu iwe ni pamoja na vifaa ambavyo kweli itaonekana kwamba jengo hili limekusudiwa kufanywa shughuli zinazohusiana na mambo ya sayansi na teknolojia kama inavyoelezwa.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo basi na kwa kuwa tunayo mifano. Tunavyo vyuo, mfano mzuri ni Chuo cha Kengeja, ambacho kwa kweli mimi napongeza sana juhudi ya walimu na wanafunzi wao kwamba wanatoa wanafunzi ambao wanapasi vizuri sana kinadharia. Lakini chuo kama kile kinakosa vifaa, sasa ikiwa bado tumeshindwa huku, sidhani kama na hiki chuo kukiambia kiwe ni cha sayansi kama kweli tutakuwa tunakwenda hivyo sambamba na hali halisi ambavyo inatakiwa iwe.

Mhe. Spika, ukiacha hapo, tunapiga kelele sana kwamba bado skuli zetu za sekondari zinakosa vifaa vya sayansi. Kwa hivyo, mimi ningeshauri kwamba haya mambo yanayohusiana na sayansi tungejaribu kujitahidi kuyatengeneza, yaani kama kuweka msingi wa kwamba hapo tutakapofikia kukiendeleza chuo kikawa sasa ni ngazi ya sayansi na teknolojia, basi iwe kweli tunao wanafunzi waliokuwa na fani ya sayansi ili kwenda kuendeleza fani zao katika taasisi hiyo. Pia, pawe na vifaa ambavyo wameanza kujifunzia kutokea chini kuanzia kwenye sekondari na vyuo mbali mbali hadi kufikia katika hizi taasisi.

Kwa hivyo, katika mtazamo wangu kuhusiana na jina la chuo, nilikuwa naona kwamba tungekuwa tunaanzia hapo kwenye *institute* ya *technology*, badala ya kwenda moja kwa moja kuanza vitu viwili kwa pamoja, na hali ya kiuwezo

bado sijaiona kama imekamilika. Hili nilikuwa nashauri sana kwamba wizara inapofikiria kufanya mambo kama haya, basi angalau iwe imejiandaa tuone kama kweli hapa sasa pameshakuwa na mwelekeo, japo si mia kwa mia, lakini angalau ikiwa imefikia asilimia 60 kwenda mbele, tutakuwa tunaweza kukifanya kile kitu *practical*.

Mhe. Spika, katika hili ninapata wasi wasi, na pengine nitaueleza vizuri huu wasi wasi ufahamike na pengine wakati waziri akitoa majumuisho tuweze kuona tumesimamia wapi.

Mhe. Spika, katika masuala mengi ya nchi yetu ya Zanzibar tunapoamua kunyanyua mguu kupeleka hatua mbele, kuna mtu huwa anatuvuta hivi, kwa maana ya kuturejesha au labda tubaki hapo hapo au turudi nyuma na si chengine ni suala zima la mambo ya Muungano.

Asubuhi hapa tumezungumza katika kipindi cha maswali na majibu kuhusiana na suala la OIC. Waziri amekiri kwamba masuala ya kiuchumi hayahusiani na mambo ya Muungano kama ambavyo sisi wengine tunaamini hivyo. Lakini bado tunalazimika kusua sua na kupiga magoti kusubiri wenzetu waridhike.

Mhe. Spika, mimi katika hili sina imani kwamba kweli kwenye masuala haya yanapokuwa yamegusa upande wa pili huwa wanazingatia upande wetu sisi. Lakini yetu sisi tu ndio huwa yanazingatia mambo yao wao, kitu ambacho mimi nakiona si sahihi na bado naendeleo kukipinga.

Tukirudi katika suala hili, Mhe. Spika, nadhani hapa itakuwa inahusiana na masuala ya elimu ya juu ambayo kwa mujibu wa Muungano huu uliopo, unaambiwa kwamba masuala haya ni ya Muungano kwa mujibu wa orodha iliyomo katika katiba hii ya Jamhuri ya Muungano na ni kipengele cha 14. Elimu ya juu ni masuala ya Muungano, ingawa kwa imani yangu mimi, mambo ya Muungano yanakomea nambari 11.

Sasa kwa kuwa hali inakwenda hivyo, “ngoma huchezwa vile inavyopigwa”. Kwa hivyo, hapa tumerudi kwamba elimu ya juu inahusiana na masuala ya Muungano. Je, tumejipanga pangaje katika kuona suala hili tutakapokuwa tunataka kulitekeleza, tunaweza kulitekeleza bila ya kuja kuambiwa subirini kwanza, maana yake kwa maslahi ya Jamhuri, sijui maslahi ya Tanzania. Hebu Mhe. Waziri akija hapa aniweke sawa hichi kichwa changu pengine hakijakaa vizuri.

Lakini Mhe. Spika, nikirudi katika waraka huu wa mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Inasema hapa mara tu baada ya Mapinduzi matukufu kulianzishwa chuo, na vyuo hivi

baadae vilikuwa ni vitano kwa ujumla yake baada ya mambo ya Muungano kukamilika mwaka 1964 April, basi vilikuwa vitano vikijumuisha na vinne vya kule Tanganyika, na sisi chetu kimoja vikawa vitano na kwa wakati huo vilikuwa na hadhi sawa sawa.

Kwa hivyo, ulikuwa unaweza kusomea Arusha, Mbeya, Unguja ikawa nyote mko sawa sawa. Lakini kwa dhana ile ile ninayodhani mimi, na sioni haya kusema kwamba wenzetu hawatutakii mema, sijui kivipi vipi wakaboresha vile vyuo vyao vikawa na hadhi, na sasa hivi vinaweza kutoa Shahada na Stashahada na pengine keshokutwa tutaambiwa vinatoa na PhD, lakini sisi tumekwamia pahala ambapo tunaambiwa havina tofauti na skuli za kawaida. Ndivyo ilivyoandikwa katika ukurasa wa 2 wa waraka huu kifungu 3 (3).

Mhe. Spika, hapa pananitia mashaka sana ikiwa hapa mwanzoni mambo yamekwenda hivi na leo tuko kwenye karne mpya mwaka 2009 na sisi Zanzibar tunataka kujitanua kwenda mbele kielimu. Sambamba na hilo tuna kero la suala la muungano huu ambao hatujui tunakwenda wapi.

Mhe. Waziri atakapokuja hapa atatueleza nini, ili tuweze kuamini kwamba tunaweza kwenda nalo suala hili wakati tunakabiliwa na kero la muungano, kwa bahati mbaya sana elimu ya kinyemela sasa ni mambo ya juu**.**

Mhe. Spika, ninadhani suala hili lingeangaliwa kwa upana sana, kwa sababu huwa ninapata hofu kubwa sana wakati tunaposikia matokeo ya wanafunzi baada ya kufanya mitihani yao, basi hata somo la Kiswahili Wazanzibari wanafeli na wanapasi wenzetu ambao Kiswahili ni Lugha ya pili.

Sasa haya ndiyo mashaka yangu katika kuanzisha Taasisi hii, huu mtazamo wa muungano tutakuwa tuko wapi. Kwa hivyo, hili niliona nilizungumzie ingawa ni muda wa mwisho na mambo mengi tayari yameshazungumziwa. Lakini niliona sina budi kuyanyuka na kuzungumza kidogo kwa ajili ya kutoa maoni yangu na wala sitaki nirudi mengine.

Isipokuwa ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze katika kuianzisha Taasisi hii hatutakwazwa na suala hili la muungano.

Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii. Maelezo yangu ya mwanzo yatakuwa ni ya jumla katika masuala ya elimu hasa elimu hii ya Sayansi na Teknolojia.

Hivi sasa tunashuhudia skuli nyingi za binafsi zikiibuka, sambamba na uendelezaji wa skuli za serikali. Lakini bado tunakabiliwa na tatizo kubwa la sayansi na wala hatuna walimu wa sayansi. Tatizo hili sasa haliko katika skuli za msingi na sekondari tu, kwa bahati mbaya limehamia katika Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*).

Mhe. Spika, tulipopita na kamati tulikuta moja miongoni mwa malalamiko makubwa yaliopo pale yanahusu masuala ya sayansi, walimu ni kidogo na hata bajeti ya kuendeleza sayansi kivitendo ni ndogo mno.

Sasa suala hili ambalo limeletwa mbele ya Baraza la Kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ni jambo zuri sana na wala halihitaji mjadala katika kiwango cha maisha ya hivi sasa tunavyoendelea kiuchumi.

Lakini nina wasi wasi ambao unanifanya niwe na hofu kubwa sana. Je, masuala haya tayakuwa yakisimamiwa na wizara hii na huku kwenye Chuo cha *SUZA* kuna malalamiko haya. Kweli tutaweza kupata bajeti ya kutosha ya kuanzisha Taasisi hii na ikafanya kazi kama ambavyo inakusudiwa kufanya kazi. Hili ndilo suala kubwa ambalo mwanzo nimetaka niliulize.

Kwa hivyo, naiomba wizara itutoe wasi wasi huu. Hivi imejitayarisha vipi kuanzisha Taasisi hii na kuisimamia kifedha, ili kuona kwamba haianzishwi tu kwa kuwa tuwe na taasisi, lakini tuwe na taasisi ambayo inatoa matunda yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, suala la sayansi kwa viwango vya skuli za msingi na sekondari. Ninadhani hivi sasa umefika wakati pamoja na serikali kuruhusu kuanzishwa skuli za binafsi, lakini masharti yangewekwa kwa kuanzisha skuli za mikondo ya sayansi. Kwa sababu ninaamini jitihada inayochukuliwa na sekta binafsi katika kuendeleza elimu ni kubwa mno.

Lakini kwa kuwa tunayo mahitaji maalum ya kuendeleza wanafunzi wetu kisayansi, kwa sababu skuli nyingi sana ambazo zinaanzishwa bado hazijatilia mkazo katika malengo juu ya suala hili la sayansi. Kwa hivyo, ni vyema masharti yaanzishwe, ili wale wanaoanzisha skuli hizi wakaonekana kwamba wanao uwezo wa kuisadia nchi hii katika nyanja ya sayansi.

Mhe. Spika, nilipousoma huu mswada wa Kiingereza niliiliona suala la *tuition* katika kifungu cha 7 (f), wakati nilipouangalia wa Kiswahili sikukiona. Lakini kumbe kulikuwa na makosa ya uchapaji na kumeruka na kimeingia kwenye kifungu cha 8 kinachoelezea kuhusu Bodi ya Taaluma, baada ya kifungu cha (e) na (f) kuthibitisha viwango vya ada na mafunzo.

Ninafikiri ni suala la marekebisho, ama iwe kifungu cha 7 au 8 kwa sababu kuna tofauti kati ya mswada wa Kiingereza na Kiswahili.

Mhe. Spika, sikupata maelezo ya awali tokea juzi ulipoanza kusomwa mswada huu na wala sikutaka nitoe maelezo ambayo pengine ningelijibabaisha. Je, ni kukigeuza Chuo cha Ufundi Karume kilichopo au kuwa Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia au kuna taasisi vyengine inaanzishwa na Chuo cha Ufundi Karume kitabakia.

Suala hilo ndilo ambalo sijapata ufafanuzi wake, kwa sababu mmoja miongoni mwa wajumbe walioeleza imeonekana kama vitu hivi viwili ni tofauti, yaani Chuo cha Ufundi Karume kitakuwepo na Taasisi itakuwepo. Kwa hivyo, ninadhani ingekuwa ni busara Baraza likaelezwa kwamba hivi sasa tunakigeuza sasa chuo hiki na kukipa jina hilo au ni vitu viwili tofauti.

Sambamba na suala la kuanzisha taasisi hii, ninafikiria sana kwa sababu hivi sasa kuna matatizo makubwa ya kuwaweka wanafunzi pamoja katika madakhalia hasa kutokana na gharama. Pamoja na hayo, kuna gharama nyengine ambazo wazee inabidi lazima walipie katika elimu, na hapa hasa limetajwa suala la kuthibitisha ada. Kwa hivyo, hapa moja kwa moja kwamba hapa kutakuwa na suala la kulipia elimu hii.

Mhe. Spika, katika kuondosha matatizo ambayo hivi sasa yapo kwa wanafunzi wanaotoka Pemba ambao wangependa kusafiri na kuja Unguja kwa ajili ya kupata elimu hii. Ninadhani imefika wakati sasa kila pale tunapofungua Taasisi kwa upande wa Unguja, basi kuwe na tawi sehemu ya Pemba, ili kuondosha matatizo haya.

Kwa sababu kama hatukuwa na tawi kwa upande wa Pemba, ina maana ni kuongeza mzigo kwa jamaa wa wanafunzi wanaotoka kule, katika masuala ya kimaisha ambao watakuja hapa na kuwategemea na baadaye waweze kwenda kupata elimu katika taasisi ambayo ipo hapa.

Suala hili limekuwa likiongeza gharama za maisha kwenye familia kubwa, jambo ambalo serikali kama itazingatia na itakuwa makini zaidi kwa kuanzisha matawi ya vyuo vyetu hivi kulingana na *geographically* ya nchi yetu basi ingekuwa ni jambo la busara zaidi.

Kwa hivyo, pamoja na sifa kubwa ambazo zimetolewa kwa Chuo cha Kengeja. Chuo hicho ni kweli ninadharia kinafundisha wanafunzi na wanapata shahada zile za kidato cha nne na wanapasi vizuri zaidi.

Lakini wasi wasi wetu sisi kwa sababu hiki kilikuwa kinaitwa Chuo cha Ufundi na masomo ya ufundi hayaonekani, yaani unaweza kwenda pale na kuuliza kitu kidogo tu cha ufundi kama vile *crew driver* au *spanner* basi havionekani.

Kwa maana hiyo inaonekani mikondo yote ya ufundi ikiwemo umeme, ufundi wa majengo na wala kwenye *motor vehicle*. Kwa hivyo, ni vyema kukipa jina linalostahiki.

Kwa sababu hivi sasa kunaanzishwa Taasisi hii, kwa nini halifanywi kuwa ni Tawi la Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia. Wakati mwengine tulikuwa tukifikiria kama chuo kile hakiwezi kufanywa Chuo cha Ufundi au Sayansi na Teknolojia, yaani Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali inashindwa kukiendeleza katika mkondo huo.

Kutokana na hali hiyo basi hata kikawa Chuo cha Kilimo, yaani kiwe kinatoa elimu ya kilimo na wala sio jambo baya. Kwa sababu tunaposhindwa kutoa elimu ya ufundi, kutokana na gharama kubwa au hatuna vifaa vya kutosha.

Hivyo ni vyema kutafuta jambo ambalo ninalowezekana, ili tuweze kutoa mafunzo almradi itakuwa ni taasisi inayotoa elimu inayohitajika katika nchi.

Mhe. Spika, katika suala la vyeti ambalo nimeliona hapa. Ninapenda nifahamishwe kwamba chuo hiki kitakuwa na vyeti vyake au vitakuwa ni vile vinavyosimamiwa na Baraza la Elimu ya Taifa. Ninapenda kufahamu hivyo, kwa sababu kama ni vyeti ambavyo vitatolewa kulingana na kile kiwango cha elimu ya Baraza la Mitihani la Taifa, lazima tujidhatiti kuwa na walimu wanaofaa.

Hivi sasa inaonekana dhahiri kwamba kiwango cha wanafunzi wanaopasi katika Chuo cha Ufundi kimeshuka sana. Miaka ambayo tulisoma sisi katika Chuo cha Karume ambapo ninadhani Mkurugenzi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tulikuwa pamoja, kufeli ilikuwa ni suala la nadra na lazima niseme hivyo.

Mhe. Spika, kama utafuatilia matokeo ya miaka ya kuanzia 1975 mpaka 1980 utagundua hivi. Wanafunzi waliokuwa wakifeli pale *average* katika miaka hiyo walikuwa hawafiki 10 na hafeli kama maana anakosa cheti, lakini huyo anafeli kwa maana anayo nafasi ya kurejea masomo mawili au moja, ili aweze kupata cheti.

Kwa hivyo, chuo kile kiliiweka Zanzibar katika heshima kubwa sana ya kielimu, kiasi ambacho mwanafunzi alikuwa akitoka Chuo cha Ufundi Karume ambaye amesoma masomo ya ufundi, wakati anapokwenda Chuo Kikuu

kuchukua fani yoyote ile, basi alikuwa akipita na kupasi vizuri na huo ni ukweli. Matunda ya wakati huo tunayaona ni walimu ambao kwa kweli wamekisaidia sana chuo. Lakini bahati mbaya sana kwa miaka iliyotangulia mambo hayakuwa hivyo, yaani kupasi ilikuwa ni jambo kubwa.

Mhe. Spika, ni vyema kufanya utafiti kwa sababu hatuwezi kutoa lawama, inawezekana kuna matatizo ambayo hatujayafanyia utafiti. Kwa sababu wanafunzi wengi wa wakati huo walipasi ninaowazungumzia leo ndio walimu. Hivi ni nini kinatokea mpaka wanafunzi wetu hawapasi vizuri katika Chuo chetu cha Ufundi cha Karume kufikia katika kiwango ambacho mpaka sasa wengi wao hawawezi kupata nafasi ya kwenda Chuo Kikuu.

Kwa mfano, ninaweza kusema moja kwa moja kwamba mazingira yamebadilika, wakali ule dakhalia zilikuwepo na wasi wasi wa kusoma haukuwepo sana ni kutaka kwa mwanafunzi. Hivi sasa inaonekana dhahiri kwamba kukosa kuwaweka wanafunzi dakhalia tena ukawahudumia ni moja ya sababu kubwa sana.

Kwani huwezi kutarajia wanafunzi wapasi wakati wa saa 8 za mchana hupo dakhalia, lakini afikirie wapi pa kupata mkate na chakula cha jioni. Hili ni miongoni mwa matatizo makubwa sana ambayo yanayoikumba elimu Zanzibar na wala sio kwenye hii nyanja ya ufundi, lakini elimu kwa ujumla wake.

Kwa maana hiyo, lazima serikali ijidhatiti sana kuhakikisha kwamba bajeti ya elimu hasa katika nyanja ya sayansi inaongezeka na wala si kutajwa kwenye vitabu vyetu vya bajeti. Kwa sababu tulitajiwa bajeti kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA)*, lakini uingizwaji wa fedha ni mbovu, yaani haupo kabisa. Kwa hivyo, leo kuna malalamiko na matatizo makubwa zaidi *SUZA* kuliko ambavyo tulikuwa tunatarajia.

Mhe. Spika, ninatoa kigezo hicho cha *SUZA*, kwa sababu tunaanzisha Taasisi ya Kisayansi tusije kupata historia mbaya kama tunavyoipata hivi sasa katika Chuo cha *SUZA* kwenye sehemu hii ya sayansi.

Nikiendelea na mchango wangu ninapenda kusema kwamba viwango vyetu vya vyeti visiangalie ndani, lakini viangalie namna viwango vya wenzetu katika sehemu nyengine tujigeze. Kutokana na suala hili la kujigeza tunaweza kukaribisha kupata wanafunzi kutoka nje na wala hawatokuja mpaka wao ni cheti cha aina gani ambacho kinatolewa. Kwa kweli cheti ambacho kinakidhi mahitaji ya ndani tu, kwa hivi sasa kinaweza kisikubalike sana nje ingawaje kwetu sisi kikawa kinatutosha.

Kwa hivyo, katika masuala ya elimu ninadhani mafundi wapo, lakini waangalie namna ambavyo kweli mitihani yetu itakuwa ni *competitive*, kiasi ambacho mtu akifanya mtihani hapa ukimleta mwanafunzi kutoka nje asiwe na wasi wasi, kwamba cheti kinachotolewa hapo kiwe kina kiwango kinachohitajika kimataifa.

Mhe. Spika, sisi tumeona jitihada kubwa sana ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kupenya kwenye taasisi za fedha za kimataifa au wahisani katika kuendeleza mipango yake. Hili ni suala ambalo tunaweza kuliiga au mfano.

Kwa hivyo, juhudi inahitajika katika kupenya zaidi hasa kwa taasisi hizi za fedha ambazo zinatoa misaada kwa serikali ya muungano, kuona ni kwa kiasi gani wanasaidia Serikali ya Jamhuri ya Muungano na keki hiyo ambayo ninakwenda huko inagaiwa vipi na sisi tukafaidika kwenye chuo hiki.

Uzoefu unavyoonesha ndani ya Baraza hili ndio kila unachokijadili unaweza kupata masuala yanayohusu muungano. Kwa sababu bado hakuna mgawanyo wa haki katika mambo ya kifedha ya misaada yanayopatikana kutoka nje kupitia Mfuko wa Muungano katika kuendeleza masuala ya Zanzibar, jambo hili liko wazi kabisa. Kwa hivyo, hivi sasa ni wakati kwa serikali kuona ina mapungufu wapi. Ni serikali ya Muungano ndio ambayo inazuia au serikali yetu kwamba nayo haijitahidi kupenya na kuomba mambo haya. Kwa mle ambamo si lazima kuitumia Serikali ya Muungano, basi ni vyema Serikali ya Zanzibar ijidhatiti kupenya na kuona kwamba nayo inapata misaada hii kutoka nje.

Mhe. Spika, nimejitahidi kuzungumza kadri ambavyo ninadhani nimetoa mchango wangu. Ninapenda niseme suala hili kwa ujumla si jambo baya ni zuri, lakini lazima tuwe na nguvu za kuliendeleza, ili isionekane tunaanzisha taasisi nyingi, lakini uendelezaji wa taasisi hizo ni mbovu.

Baada ya kusema hayo, ikianzishwa taasisi hii mimi nitakuwa wa mwanzo kupeleka wanafunzi na kwa hivyo ninaitakia kheri ianze na iendelee, ili iweze kutoa faida inayokusudiwa.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana (*Makofi*).

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kusimama hapa na kuweza kuchangia mswada huu muhimu katika ujenzi wa taifa letu, ambao unahusu kuanzishwa kwa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo ya mwaka 2009.

Kwanza ninawashukuru wajumbe wote ambao walipata nafasi ya kuchangia na kutoa maoni pamoja na ushauri wao. Mhe. Spika, inaonesha dhahiri kwamba wajumbe wameridhika na mswada huu na wengi wao wameunga mkono kuanzishwa kwa taasisi hii.

Mhe. Spika, mbali ya maoni yao kuna baadhi ambao walikuwa na hofu ya kuanzishwa kabla hatujajitayarisha, lakini ninaamini kwamba jambo hili wanaliona ni zuri kwa kuanzishwa.

Vile vile kuna wajumbe ambao wanadhani ni vyema kwanza kuanzishwa taasisi inayohusiana na teknolojia badala ya kwenda moja kwa moja na kuanzisha taasisi inayohusiana na sayansi na teknolojia.

Mhe. Spika, pia wapo ambao walikuwa na hofu ya kuona jinsi gani tumejitayarisha katika kuanzisha taasisi hii, kwa maana ya kwamba matayarisho ya vifaa pamoja na huduma nyengine ambazo zinahitajika.

Mhe. Spika, napenda nianze kwanza kuwatoa hofu Waheshimiwa Wajumbe kwamba serikali imejiandaa na imeona umuhimu wa kuanzisha jambo hili. Mhe. Spika, kwanza napenda nitoe maana kama nilivyoinakili, maana ya sayansi pamoja na maana ya teknolojia.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa nakala niliyoipata ni kwamba sayansi ni taaluma ambayo inahusiana ama na miundo ama na tabia za ulimwengu ambayo tunasema ni vitu vilivyomo katika ulimwengu, ama vitu hivyo vitakuwa ni vitu vya maumbile ama vitu ambavyo vimetengenezwa. Lakini hiyo inategemea vile vile na ukweli ambao unaweza ukauhakikisha kwa njia ya kufanya majaribio. Kwa Kiingereza wanasema ni:-

> *"knowledge about the structures and behaviour of the natural and physical one based on the facts that you can prove experimentally or by experiment."*

Lakini ukija kwenye suala la teknolojia nalo linahusiana vile vile wanasema ni *"scientific knowledge used in practical ways in industries."*

Yaani hii inahusiana na sayansi, huwezi kuwa na teknolojia bila ya kuwa na sayansi. Kwa maana nyengine ni kwamba ili uweze kuwa na teknolojia unahitaji sayansi. Kwa sababu ni mambo ambayo yanakwenda sambamba.

Mhe. Spika, kwa maoni yangu mimi naona ni kwamba huwezi kuwa na teknolojia bila ya kuwa na sayansi. Kwa maana hiyo, ni dhahiri kwamba suala la sayansi na teknolojia linakwenda sambamba.

Mhe. Spika, suala la kujitayarisha, ni vyema kwamba tukalifikiria tumejitayarisha vipi katika kuanzisha taasisi hii. Mhe. Spika, kama tutakuwa na kumbukumbu huko nyuma tunakotoka kabla ya uhuru wa nchi hii, watu walikuwa na wasi wasi jinsi gani tunaweza tukaiendesha nchi hii. Pia wapo ambao walitoa wasi wasi wao kuona kwamba pengine kwa kipindi kile haukuwa wakati muafaka kupata uhuru mpaka tujitayarishe tusome tuwe na taaluma nzuri nzuri ndipo ambapo tudai uhuru.

Mhe. Spika, hii imekuwa baada ya uhuru kwa mfano, imedhihirisha dhahiri kwamba kumbe mawazo yale ya kwamba ni lazima kwanza tujitayarishe tuwe na taaluma ambayo iliyobobea halafu ndipo tupate uhuru, inaonekana kwamba haikuwa sahihi kwa upande mmoja. Kwa sababu uhuru tulioupata watu wetu wengi walikuwa bado hawajakuwa na taaluma kubwa, lakini maendeleo ambayo tuliyapata baada ya uhuru yalionesha dhahiri kwamba tungeweza kufanya kitu hata kama hatukuwa na taaluma kubwa kama tulivyofikiria mwanzo.

Mhe. Spika, nitoe mfano mwengine wa wazee wetu hapo nyuma. Zamani mtu alipokuwa anataka kuoa anaambiwa chukua mkoba ndani yake kuna kuku pengine na kanzu. Lakini kumbe anapoondoka pale hajui safari ile anakwenda wapi. Akifika kule anapewa mke anaoa na hatimae anaishi na kuendesha maisha yake na kuzaa watoto.

Mhe. Spika, mfano mwengine mimi ambaye pengine nilikuwa ni kijana wa sasa, nilikuwa na hofu zaidi pengine nilipoambiwa nioe kutokana na kwamba sijajitayarisha. Lakini kumbe baada ya kuoa unaona kwamba maisha yanakwenda vizuri kuliko vile ambavyo ulivyofikiria mwanzoni kwa kuwa hujajitayarisha.

Mhe. Spika, hii ni mifano tu ambayo inaonesha kwamba matayarisho yanaweza kuja baada ya kufikiria. Kwa sababu lazima kwanza uwe na nia au uwe na dhana ya kuweza kufanya jambo ndipo baadae jambo lile linaweza kufanyika.

Mhe. Spika, mswada huu wa sheria ni moja ya matayarisho ambayo serikali inajitayarisha katika kuhakikisha kwamba suala hili linafanikiwa. Mhe. Spika, ni lazima kwanza ama uwe na sera au uwe na sheria ndio ambayo yataweza kukuongoza katika kufanya jambo. Huwezi tu ukafanya jambo bila ya kuwa na sheria ama sera ya kuweza kufanya jambo lile.

Mhe. Spika, napenda niwatoe hofu kwamba mswada huu wa sheria ni moja ya matayarisho ya serikali katika kuona kwamba taasisi hii itakwenda kama ilivyopangwa. Mhe. Spika, sheria ni mwongozo unaoweza kuelekeza wapi tutakwenda na tatizo likitokea tufanye nini.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba niende moja kwa moja kwenye mswada ili nichangie na kutoa maoni yangu. Lakini kabla sijachangia kwanza napenda niunge mkono mswada huu mia juu ya mia na na ninautakia kheri ili uweze kufanikiwa.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 6 sehemu ya 3, waheshimiwa wengi wamekigusia jinsi kinavyoonekana hapa. Mhe. Spika, kifungu hiki kinahusiana na jinsi waziri atakavyoteua wajumbe 5. Inaonekana dhahiri hapa kwamba wajumbe ni 8 badala ya 5. Hii inaonesha kwamba kuna makosa ama ya uchapaji au makosa mengine. Lakini hapa baada ya ile namba ya kirumi ya (v) ambayo inayofuatia inakuwa ni (d), (e) na (f) ndivyo ilivyo. Kwa maana hiyo, wajumbe ni 5, ni kuanzia kifungu cha 1 mpaka kifungu cha 5. Kwa hiyo, napenda wajumbe wafahamu hivyo kwamba hapa inaonekana kuna marekebisho.

Lakini jengine Mhe. Spika, ambalo limejitokeza katika mswada huu, wajumbe wamehoji kwamba kulikuwa na makosa mengi ya uandishi na kwa nini imepitia katika mikono mbali mbali na makosa haya hayajaonekana.

Mhe. Spika, wanaopitia mswada huu ni binadamu na kama binadamu, basi anaweza akapitikiwa na yeye anaweza asiyaone mambo. Lakini pengine kwa sababu ya ubinadamu haya ndio yametokea. Kwa hivyo, mengi yamerekebishwa kwa yale ambayo yanaonekana ni makosa, basi Kamati ilipokaa mara ya mwisho iliyaona na kufanya marekebisho.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo limejitokeza ni kuhusu masomo ya sayansi katika maskuli yetu. Wengi wa wajumbe wameonyesha hisia zao za kuona kwamba ingekuwa busara zaidi kwamba tukaweza kujifunza masomo ya sayansi katika skuli zetu za kawaida, na baadae ndipo tukaanzisha taasisi hii, pamoja na kwamba bado tuna kasoro katika maskuli yetu, lakini bado vijana ambao wanafaulu na wanahitaji kuendelea mbele katika masomo haya ya sayansi na teknolojia.

Kama hatutowatayarishia mazingira mazuri hawa wachache ambao tunawapata sasa hivi, basi tutaendelea kuwa na kasoro hizo, kwa maana kwamba hatutoweza kupiga hatua ile ambayo tunaitaka, lakini ni vyema hawa wachache tulikuwa nao hivi sasa ambao wanafaulu vizuri, wakapata fursa ya kuweza kuendelea katika vyuo ambavyo vina hadhi inayotakiwa.

Mhe. Spika, pamoja na kasoro hizo, lakini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali bado inaona kwamba inachukua jitihada kubwa katika kuhakikisha kwamba inaweka mkazo katika masomo haya ya sayansi ambayo ni msingi katika chuo chetu kama hichi wakati kitakapoanzishwa.

Sasa baadhi ya jitihada ambazo serikali inachukua ni kuona kwamba vile vifaa pamoja walimu na mambo mengine yanayohusiana na masomo ya sayansi yanapatikana. Mfano mzuri ni kwamba hivi sasa nadhani hakuna tatizo la vitabu vya sayansi, vitabu vipo kuanzi darasa la tisa hadi darasa la kumi na nne. Ninaamini kabisa kwamba vitabu hivyo vinatosheleza katika kuwaendeleza vijana kwenye masomo yao. Tunalo tatizo la walimu kama walivyoonyesha hofu waheshimiwa wajumbe na hili Wizara inachukua jitihada za kuona kwamba tatizo hili nalo linapata ufumbuzi. Watu wanasema, mwendo wa hatua mia huanza na hatua moja. Hapa tunapoanza ni ishara ya kwamba tunaendelea mbele na ni ishara ya kwamba tutafanikiwa.

Jambo jengine ambalo limejitokeza ni suala la bajeti ya Elimu kupewa mkazo. Naamini kabisa nyinyi ndio wajumbe ambao mnao mchango mkubwa katika kuhakikisha kwamba bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inakua, au inafikia pale ambapo panahitajika. Tunawaomba sana wakati wa bajeti mtusaidie na muweze kuipa nguvu bajeti hii, ili iweze kupata nguvu ya kuweza kufanikisha yale ambayo yanapangwa.

Mhe. Spika, wajumbe pia wameonyesha hofu yao au wameshauri kwamba kuweko na mipango mizuri ya kuhahikikisha kwamba haya tunayoyapanga yanaweza kufanyika vizuri. Nakubaliana nao kwamba bila ya mipango mizuri basi hakuna kitakachoweza kufanikiwa hata kama utakuwa umekiandaa vizuri gani. Lakini kama hutokuwa na mipango mizuri ya utekelezaji, basi bila ya shaka mpango huu hautofanikiwa.

Moja ya suala ambalo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaliona lina umuhimu mkubwa ni kuona kwamba inaandaa mipango ambayo inatekelezeka, mipango ambayo inaweza kufikia malengo yanayohitajika. Nina uhakika kabisa kwa wataalam tulionao, Wizara ya elimu na tasisisi mbali mbali kwamba wanaweza wakafanya vizuri katika kufanikisha mipango hii ya maendeleo.

Mhe. Spika, suala la walimu nalo limekuwa ni suala ambalo limezungumziwa sana, na wajumbe wameonyesha kwamba kuna haja ya kuwa na walimu wa kutosha na wenye sifa ambao wataweza kufanikisha taasisi hii. Hivi sasa kuna taarifa kwamba wapo ma-*doctor* ambao wamemaliza masomo katika fani hizi za sayansi na teknolojia ambao bado wana hamu ya kufundisha chuo hiki. Mimi binafsi tayari nimeshapata maombi ya kuona kwamba kuna watu ambao wanataka kujiunga na taasisi hii ambao pia nao wamesoma katika chuo hicho hicho, na wanaona umuhimu na uzalendo wa kuendeleza taasisi hii. Tunao watu kama hao na naamini kabisa tutawatumia katika kuendeleza taasisi hii.

Suala jengine ambalo limejitokeza ni kuhusu jina la mswada, kuna baadhi ya wajumbe wameona kwamba jina la mswada liko kinyume nyume. Wanauliza kwa nini lianze jina la Karume halafu sayansi na teknolojia. Wakati wa kujadili mswada huu kwa mara ya mwisho hili tuliliona na tukaona kwamba ni sahihi, jina liko sahihi na bahati nzuri mara hii kamati hii ya maendeleo ya wanawake na ustawi wa jamii ina wajumbe madhubuti ambao wamebobea katika suala la lugha ama ya Kiswahili ama ya Kiingereza. Mhe. Spika, hapa nina uhakika tulipata ushauri mzuri kwa kuona kwamba jina hili ni sahihi na jina ambalo liko vizuri.

Mhe. Spika, kuna mambo mengi ambayo yamejitokeza katika mswada ambayo tunahitaji kuyazingatia, kama Wizara tutajitahidi kwamba yale maoni na ushauri mliotupa tutauchukua na kuufanyia kazi.

Lakini kuna baadhi ya wajumbe wamehoji kwamba ni sayansi gani ambayo tunaihitaji. Sayansi imegawika katika mafungu mbali mbali, kuna sayansi inayohusiana na viumbe, kuna sayansi ambayo inahusiana na madawa, kuna sayansi ambayo inahusiana na ardhi, kuna sayaansi ambayo inahusiana na mambo ya anga. Sayansi zote hizo sisi tunazihitaji na ndio maana tukasema tuanzishe Chuo cha Sayansi na teknolojia kwa maana ya kwamba sayansi zote tunazihitaji, tunahitaji sayansi ambayo inahusiana na viumbe, tunahitaji sayansi ambayo inahusiana na madawa, tunahitaji sayansi ya kila kitu.

Mfano tunahitaji sayansi ya kurusha ndege wanafunzi ambao watasoma katika taasisi hii naamini kwamba watapata fursa mbali mbali za kujiendeleza katika nyanja mbali mbali, kwa hivyo itawajengea msingi wa kuona kwamba huko mbele wanaweza kujitanua katika sehemu gani ambayo wanahisi wanaweza kufanya vizuri.

Kwa hivyo, hii ni taasisi ambayo inawaandaa wana sayansi na wana teknolojia kwa maana ya kwamba nyanja mbali mbali ambazo wataamua baadae kujiendeleza waweze kujiendeleza, hatuwezi kujikita katika eneo moja tu la sayansi kwa sababu tuko katika ulimwengu ambao tunayahitaji yote, taasisi hii kama nilivyosema kwamba ni taasisi ambayo itaandaa vijana halafu baadae wataweza kutawanyika katika maeneo mbali mbali ya sayansi.

Mhe. Spika, mjumbe aliyeuliza hivi alikuwa na maana kwamba kama tutakuwa tunahitaji sayansi ya kutengeneza vitu. Baadae akahoji kwamba tutakula hasara kubwa kwa sababu hatuna mali ghafi. Nitoe mfano kwa nchi ya Msumbiji, ni nchi ambayo ina kiwanda kikubwa cha kutengeneza *alluminium* na hawana mgodi wa kuchimba *alluminium* Msumbiji, isipokuwa mali ghafi zinatoka Marekani, Japan na zinatoka Australia. Naambiwa kwamba katika kutengeneza *alluminium* kuna vitu vitatu ambavyo vinahitajika kutengeneza hiyo

alluminium. Nilipata bahati ya kutembelea kiwanda hiki ambacho kinaitwa MOZALE, lakini wanaoendesha kiwanda hiki wanachukua mali ghafi Australia, wanachukua Marekani na Australia na Japan baadae wanafanya pale na kuweza kupata *alluminium.* Walichokifuatia pale ni umeme na wafanyakazi.

Mhe. Spika, nchi ya Msumbiji imebahatika kuwa na umeme mwingi, kwa kuwa kiwanda hiki kinahitaji umeme mwingi wakaona ni sehemu ambapo wakakae kwa kuendesha shughuli zao, lakini suala la malighafi pale hawana. Sasa hata na sisi tunaweza kubuni kiwanda ambacho hapa kinaweza kuendelea, ili uweze kuendesha kiwanda unahitaji mambo mengi, hata wafanyakazi wana mchango mkubwa wa kuweza kuendesha kiwanda, kama kuna wafanyakazi ambao utawapata kwa bei nafuu, basi ni moja ya sababu unayoweza kuitumia kuendesha shughuli yako.

Mhe. Spika, tumekuwa tunazungumza hapa Barazani kwamba tuna mafuta, lakini mafuta haya tunashindwa kwa sababu ya teknolojia. Lakini kama kutakuwa na taasisi ambayo itakuwa inafundisha vijana wetu tunaweza kutumia teknolojia hiyo na kuweza kuchimba mafuta yetu. Mimi binafsi basi naona taasisi hii ni muhimu mno katika maisha yetu na nina uhakika kama tutakuwa na nia, basi tunaweza kufanya vizuri sana katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda na kwa sababu mimi natakiwa nichangie kijumla jumla nimpe nafasi Mhe.Waziri aweze kuja na hoja za mjumbe mmoja mmoja. Sasa naomba niishie hapo na kwa mara ya pili niseme tena naunga mkono mswada huu wa kuanzisha taasisi ya Sayansi na teknolojia kwa mwaka 2009. Mhe. Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, na mimi sina budi kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nikazungumza machache katika kuchangia mswada huu wa kugeuza Chuo cha Ufundi cha Karume kuwa Chuo cha Karume Sayansi na Teknolojia, mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuweza kuona umuhimu wa kuleta mswada huu wa kuweza kufanya marekebisho ya kuendesha kile chuo.

Mhe. Spika, kama walivyosema baadhi ya wajumbe kwamba Chuo cha Karume ni chuo ambacho cha muda mrefu sana, chuo ambacho kimeweza kututolea wataalam wengi katika miaka ya nyuma na kilikuwa ni chuo cha kujivunia sana hapa kwetu. Kimsingi miongoni mwa baadhi yao huwemo hata ndani ya Baraza hili. Kwa hivyo, baada ya miaka mingi kupita na kuona kwamba sasa hivi dunia imebadilika, lakini vile vile na uwezo wa kuendesha chuo kile katika hali halisi iliyopo sasa hivi tutakuwa tunakosa yale matunda ambayo tulikuwa tunayategemea yaendelee kupatikana katika chuo kile.

Kwa hivyo, kuletwa kwa mswada huu ni moja katika mbinu au mikakati ya serikali kuhakikisha kwamba chuo kile bado kinaendelea kuwa na hadhi ile ambayo ilikuwepo zamani. Kumekuwa na mawazo tofauti tofauti katika uchangiaji wa mswada huu, lakini tofauti hiyo ya mawazo yote ilikuwa inalenga katika kuboresha huu mswada, na katika mambo mengi ambayo yanaulizwa hakuna mtu ambae ameupinga, isipokuwa watu walikuwa wanaelezea zaidi hofu. Kuwa na hofu sio tatizo sana kwa sababu ukiwa na hofu ndio unataka kujihakikishia kwamba kile ambacho kinafanyika au kinataka kufanyika kweli kitakuwa katika hali halisi iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, tulipokuwa tumeanzisha vyuo mfano kama Chuo Kikuu cha Zanzibar yaani *SUZA* kulikuwa na hofu nyingi ambazo tulikuwa nazo hapa, lakini kimsingi sasa hivi tumeanza kuona matunda yake. Chuo kila siku kinaimarika na wanaingia wanafunzi na wanatoka wale waliokuwa tayari wataalam katika sehemu mbali mbali. Kwa hivyo, ile hofu ya kwamba tutakuwa na uwezo wa kuendesha kile chuo wataalam tutawapata wapi haipo.

Sasa hofu iliyokuwepo katika kuanzisha *SUZA* baadhi ya waheshimiwa wamezungumzia tena katika uanzishwaji wa chuo hiki, kwa hivyo mimi nilikuwa najaribu kumpongeza Mhe. Waziri kwa sababu amekuwa na hofu sasa hata kile anachokifanya anakuwa anakifanya kwa uhakika na ile hofu waliyokuwa nayo waheshimiwa ndani ya utendaji wake, basi inaondoka kidogo kidogo. Kwa hivyo, tunategemea baada ya kupitishwa sheria hii chuo kitakuwa na uwezo mzuri zaidi kuliko ambao kinao sasa hivi.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya hofu ambayo ilikuwa inaelelezwa kwamba labda bajeti ya serikali ukiangalia sasa hivi katika wizara ambazo serikali inajitahidi kuiwangizia mafungu yao kwa vizuri zaidi, basi ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kama sio ya mwanzo basi ya pili, kwa hivyo serikali kwa upande wake inajitahidi sana kuongeza nguvu hasa kwa kupitia Wizara ya Elimu. Kwa hivyo tunapokuwa tunaanzisha vyuo kama hivi, basi na nguvu zaidi serikalini inategemea tutaweza kutoka na kuona vyuo vyetu vinaimarika.

Lakini vile vile katika mbinu za kuweza kuboresha hivi vyuo moja ni kuleta huu mswada kama Mhe. Abass Juma Mhunzi alijaribu kuelezea, kwamba kutokuridhika na lile gawio ambalo tunalipata pengine katika miswada ya nje, na mbinu gani serikali itafanya kuweza kuhakikisha kwamba tunaweza kupata fungu zaidi. Kwa hivyo, moja katika mbinu ya kuweza kupata fungu zaidi nje ya ile ambayo tunapata gawio letu kupitia ile 4.5, basi moja katika mbuni nyengine ya serikali ndio hii. Kwa sababu katika sheria hii nafikiri tukiangalia kwenye sehemu ya 4 ya mswada pale panaelezea masharti ya fedha.

Kwa hivyo pale katika sehemu ya 4 panapoelezea masharti ya fedha kuna fedha za taasisi, Mhe. Spika, naomba ninukuu.

Kifungu cha 14 kinaeleza.

"Fedha na mapato ya taasisi yatakuwa"

a) "Fedha zile ambazo zitatolewa na serikali kwa ajili ya Taasisi"

Kwa hivyo ni fedha ambazo zitolewa na bajeti yenyewe ya serikali.

b) "Fedha zile ambazo Baraza, mara kwa mara linaweza kukopa kwa ajili ya Taasisi"

Kwa hivyo ina maana baraza lenyewe la chuo litakuwa na nguvu ya kisheria ya kuweza kukopa fedha kutoka taasisi yoyote ya serikali au binafsi kuweza kukipa nyenzo kwa kukipa nguvu hiki chuo.

Imeendelea huku mbele na kusema kama ifuatavyo:

c) "Misaada na michango kutoka taasisi au kwa watu binafsi"

Kwa hivyo ndani ya sheria hii imetoa nafasi ya kwamba chuo kuweza kuwa na mamlaka kubwa ya kuweza kujiendesha pengine ilivyokuwa hapo mwanzo, sasa ile hofu ambayo tulikuwa tunadhania na tunategemea kwa kuwa kutakuwa na Baraza la Chuo kutakuwa na watu wenye upeo mkubwa, watakuwa na taaluma kubwa vile vile. Lakini na kuweza kuangalia ni maeneo gani wanaweza kupata misaada kwa kuweza kukiendesha chuo kwa vizuri zaidi, kama hofu ni kwa walimu bado katika kifungu cha 12 pale imeelezwa uajiri wa wafanyakazi naomba kunukuu.

Kifungu cha 12 kinasema:-

> "Baraza kwa mujibu wa masharti ambayo yataonekana yanafaa, litaajiri idadi ya wafanyakazi katika kada ya taaluma na isiyokuwa ya taaluma ya Taasisi".

Kwa hivyo, bado Baraza litakuwa na uwezo wa kuweza kutafuta walimu watakaoweza kuja kutoa ile *product* itakayokuwa inahitajiwa katika chuo. Mimi nadhani ile hofu waliyokuwa nayo, wasiwa na wasi wasi na kama vilivyoanzishwa vyuo vyengine tukaanza kuwa na mashaka, lakini sasa hivi vyuo vile vinakwenda vizuri sana.

Labda kuna suala moja ambalo Mhe. Waziri ambalo Wazanzibari wengi huko nje huwa wanajiuliza uliza, ukiweza kutupa ufafanuzi utakuwa umewasaidia watu wengi zaidi, kwa sababu inawezekana ikawa wanajua watu wachache, lakini wengine wakawa hawajui itazidi kutudhibitishia huu uhalali wa vyeti vyetu ambavyo vinavyotolewa na vyuo vyetu vikuu hapa Zanzibar, kuna wengine wamekuwa na hofu wanasema elimu ya juu ni mambo ya Muungano, sasa Zanzibar sijui tuna vitu gani. Sasa hiki ukijakukielezea kitazidi kuwaamsha na kuwapa taaluma Wazanzibari kwa kujua humu wanamopeleka watoto wao, basi vile vyeti wanavyopata vitakuwa na nguvu gani, au vinatambulikana namna gani huko duniani.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa sina mchango mkubwa sana, isipokuwa kuja kum-*support* Mhe. Waziri kwa kuleta mswada huu, ambao tunategemea sasa hivi kutakuwa na mabadiliko makubwa katika chuo chetu cha Karume. Kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwamba sayansi ina uwanja mpana, kwa hivyo tunategemea tutaanza kupata mabingwa wa aina tofauti tofauti ambao watazalishwa hapa Zanzibar, kwa kuwa sasa hivi tunaingia soko la Afrika ya Mashariki pamoja na kelele zetu tunazopiga, lakini ndio tunaelekea huko.

Kwa hivyo, moja katika mbinu ambayo tunatakiwa tujiandae Wazanzibari tusiwe watu wa kulalamika tuwe watu wa kujiandaa zaidi. Tukiweza kupata wataalam wazuri, basi zile nafasi ambazo pengine zilikuwa zije kuchukuliwa na watu kutoka sehemu nyengine ya Zanzibar tutakuwa tayari tumeweza kutengeneza wataalam watakaoweza kushika nafasi mbali mbali katika taasisi zetu za hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa hivyo mimi pamoja na wananchi wangu wa jimbo la Kwamtipura tunaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kutoa hoja kwamba uliahirishe Baraza lako tukufu kabla ya muda wake mpaka Saa 11.00 jioni.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe sasa niwahoji waliofiki wanyanyue mikono na wasiokubali, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
(Saa 5.50 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kujadili Mswada wetu huu na hatimaye leo kufika wakati huu nikaweza kutoa majumuisho haya tukiwa na afya njema.

Mhe. Spika, naomba kwanza uniruhusu niwataje wale wote ambao walibahatika kuchangia, sikupata mchangiaji kwa njia ya maandishi wote waliochangia walichangia kwa kusema nao ni kama hawa wafuatao:

1. Mhe. Ali Suleiman Ali — Mwenyekiti wa Kamati
2. Mhe. Mohammed Ali Salim — Wazi Kivuli
3. Mhe. Said Ali Mbarouk
4. Mhe. Hamad Masoud Hamad
5. Mhe. Rashid Seif Suleiman
6. Mhe. Mzee Ali Ussi
7. Mhe. Ali Denge Makame
8. Mhe. Haji Faki Shaali
9. Mhe. Asaa Othman Hamad
10. Mhe. Suleiman Hemad Khamis
11. Mhe. Abdulla Juma Abdulla
12. Mhe. Haji Mkema Haji
13. Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim
14. Mhe. Omar Ali Jadi
15. Mhe. Ame Mati Wadi
16. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
17. Mhe. Ali Abdalla Ali
18. Mhe. Zakiya Omar Juma
19. Mhe. Abassi Juma Muhunzi
20. Mhe. Khamis Jabir Makame na
21. Mhe. Hamza Hassan Juma.

Jumla ya wachangiaji walikuwa ni 22. Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wizara kwa kuwashukuru sana kwa michango yao mbali mbali ambayo imetusaidia sana na itatusaidia kwa pamoja.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Ali Suleiman Ali na kamati yake. Walitushauri, walituongoza na baadaye waliwasilisha ripoti yao hapa. Pamoja na masahihisho yote tumeyafanyia kazi na Ishalla tutakwenda kuyafanyia kazi zaidi. Naomba nimpongeze Mhe. Ali

kwa sababu nimegundua kwamba anasoma vitabu vingi sana, kwani kawanukuu wataalamu wa kutoka India waliozungumzia uchumi wa India na akatafsiri na akasema naomba ninukuu kidogo. Alikuwa anatafsiri maana ya sayansi na teknolojia, hawa ni Wahindi Dats na Sundaram.

> "Anasema sayansi na teknolojia ni njia aitumiayo mwanadamu katika kuyabadilisha mazingira yake"

Hili ni neno kubwa sana na akatoa ufafanuzi baadaye. Kwa ujumla namshukuru sana na namuahidi ushauri mbali mbali aliotushauri katika kuuweka Mswada wetu kuwa mzuri zaidi tutafanya hivyo.

Mhe. Spika, vile vile nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumshukuru Waziri Kivuli. Alituasa mapema kwamba tuwe watulivu, wasikivu ili kuweza kumsikiliza. Tumejitahidi kuwa wasikivu na watulivu na tumemsikiliza mwanzo hadi mwisho. Bahati nzuri safari hii hakuwa na mengi, yalikuwa ni mafupi lakini yalikuwa ni mazito.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kwa wajumbe wote 22 waliochangia kwa dhati kabisa na kwa imani kubwa sana walichangia wote kwamba jambo hili waliliona ni zuri si baya, lakini walikuwa wanatushauri tuwe na hadhari katika kulianzisha jambo hili. Binaadamu yeyote ambaye anampa tahadhari mwenzake basi anampenda. Lako wewe ni kulizingatia lile ambalo mwenzako amekwambia. Waheshimiwa hawa wote walitushauri ipasavyo na wakatueleza kwamba jamani liangalieni vizuri hili suala ni zuri sana, hakuna hata mmoja wetu ambaye analipinga suala hili. Yote yale tumeyachukua kuwa ni mapenzi na furaha kwetu sisi kwamba wenzetu walikuwa wanatushauri hapa na pale. Zile hofu zilizotolewa walikuwa wana wajibu wa kuzitoa na mimi nitajitahidi kuzipunguza inawezekana nikawa nisizamalize kabisa.

Mhe. Spika, kwa ujumla naomba niwatoe mashaka makubwa kwamba Chuo cha Karume hivi sasa lile wazo ambalo limetolewa na Waheshimiwa Wajumbe nadhani Mhe. Said Ali Mbarouk na Mheshimiwa mwengine alipendekeza kwamba nivizuri kamati kama hizi zinapopitisha Miswada kama hii ambayo kwa hatima ya baadaye wangepata fursa kutembelea zile taasisi.

Mimi nashauri pamoja na kwamba kamati imefanya kazi yake, lakini wangekwenda Chuo cha Karume sasa hivi wakaone kuna mambo gani ambayo yametendeka pale na haya matayarisho tunayoyakusudia yapo vipi. Hivi ninavyozungumza sasa hivi Chuo cha Karume kina watu ambao wana *masters* kwenye taaluma mbali mbali za kiufundi ambao wapo tayari. Hivi sasa karibu watu 18 wapo, wawili ambao wanachukua PhD wako nje. Baadaye takwimu hizi nitazitoa wakati nitakapojaribu kutoa ufafanuzi wa hapa na pale.

Mhe. Spika, Mhe. Mula katika mchango wake alituwasa sana na akatuuliza maswali kwamba uwezo tunao? Uwezo tunao kwa sababu takwimu hizi ambazo ziko hapa zinaonesha wenye *degree* ya kwanza ni 13 wapo Chuo cha Karume sasa hivi.

Kwanza ni lazima tujue walimu kama wapo, wapo wa *degree* ya kwanza, wapo wenye *CIVIL , Engineering, mechanical engineering, electrical engineering*, kwenye *telecommunication,* na mengine ya jumla. Wenye *degree* ya pili wapo 9 jumla hapo ni 22, ukiacha wale wenye advance diploma ambao tunao 26 jumla ni 48. waliokuwepo masomoni na ambao wengine hivi karibuni watarudi wenye digrii ya kwanza ni 5 na *degree* ya pili ni 9 na *PhD* yaani digrii ya tatu ni 2, kwa masomo haya. Hata tulipoanzisha SUZA, basi hatukufika kiwnago hiki na tunashukuru hali ni nzuri. Baadaye nitazungumzia suala la SUZA kwani Mhe. Muhunzi na Mhe. Haji Faki walilizungumzia sana suala la SUZA na bajeti zake.

Ninachoweza kusema kwa ujumla ni kwamba *degree* sio lazima uitoe kwenye jengo zuri sana. *University* zote duniani na nyengine nyingi zilianza katika majengo ya muda tu. SUZA tumeanza na majengo ya muda ukiacha Chukwani na Zanzibar *University* ambao walijenga majengo mapya. SUZA tulianza na jengo la Taasisi na lilikuwa ni bovu. Baada ya kupata bajeti zao wakaanza kutengeneza na sasa hivi tunamshukuru Mwenyezi Mungu, mikupuo mitatu imeshamalizika na wanaendelea kutengeneza. Tunashukuru kidogo hali ya SUZA ni nzuri.

Mhe. Mulla katika mchango wake alisema kwamba tusimuige ndovu. Sasa sifa za ndovu sijui tumuige kwa kitu gani, maana ndovu ana sifa nyingi. Kwanza ni mnyama mkubwa na mengineyo. Lakini kama unahisi mwenendo wa ndovu unaweza angalau ukafika robo yake au nusu yake basi usivunjike moyo. Mimi nasema tujaribu na tusijaribu kwa kubahatisha tu, bali tujaribu kwa uhakika.

Mheshimiwa uliposema kwamba Wizara ya Elimu ina matatizo mengi, miye sikatai. Na kama siku itatokezea duniani au siku itatokezea kwamba wizara yangu ikawa haina tatizo hata moja itakuwa dunia tena ndio imefika siku yake ya mwisho. Matatizo yapo hata kwenye familia.

Naomba nitoe mfano kidogo. Ndani ya nyumba bwana na bibi wanaweza wakatofautiana kidogo. Bahati nzuri akitokezea mgeni ndio panakuwa na manusurina ule ugomvi unakwisha kwa muda. Sisi wanaume huwa tunapenda yule mgeni asiondoke maana yake akiondoka tu mambo yanakuwa yapo pale pale. Sasa yale ni matatizo ya kifamilia yapo siuze taasisi kubwa kama Wizara ya Elimu inawafanya kazi zaidi ya elfu kumi na nne (14,000). Tumeweka

wakurugenzi, walimu wakuu, maafisa wa elimu Wilaya, maafisa wa elimu Mkoa ili kupunguza hayo matatizo.

Baraza la Wawakilishi kuna Kamati ya Maendeleo ya Jamii, moja katika jukumu lake ni kutusaidia. Nashukuru sana kamati safari hii ilipokuja imetusaidia mambo mengi sana. Walikuwa wanatupa ushauri wa hapa na pale pa kupongeza walipongeza na pale pa kutuelekeza walituelekeza. Sidhani kama watakapokuja tena kama hawatokuja na mambo mengine ya kutuelekeza. Siku ile wangelikuwa wakinielekeza kama ningewambia sikilizeni bwana, miye sifanyi chochote hapa nilipofika ndio hapa hapa ningekuwa sina maana. Nilikuwa mtiifu kweli kweli kwa sababu sitaki kuja kuwekewa vikwazo huku ndani ya Baraza na nitaendelea kuwa mtiifu. Sisi tunafanya kazi kwa kushirikiana na waheshimiwa hawa.

Mhe. Mohamed Salim (Mulla) pamoja na *comment* zako nyingi lakini nakushukuru. Majengo pia umesema mabovu, umetaja Utaani, umetaja Fiedel Casro, Lumumba, Kengeja hii ndio imetajwa sana. Kwanza nataka niseme kwamba Kengeja sio *College* hii ipo kwenye *level* moja na ya Mikunguni ni *Technical Secondary School*. Nakiri kwamba kweli Kengeja kuna matatizo na tunayajua na sio Kengeja tu ni mwahali mwingi tu. Mimi nawapongeza sana walimu wa Skuli ya Kengeja ya Sekondari pamoja na matatizo waliyokuwa nayo, lakini wameweza kuchukua nafasi ya kwanza kwa baadhi ya masomo kwa Tanzania nzima. Naomba tuwapongeze sana walimu wetu wa Skuli ya Kengeja. Leo hii nimemwita mwalimu wa Chuo cha Karume, nikamwambia tunaanza kuupeleka Mswada huu kupandisha daraja hizi ni *Technical Secondary Schools* moja ipo Mikunguni na nyengine ipo Pemba Kengeja.

Mikunguni na Karume wameanza kuanzisha baadhi ya vifaa vya ufundi wao wenyewe. Sasa tumemtaka Mkuu wa Chuo cha Karume na wenzake waende Kengeja wakaonane na Mkuu wa Chuo kile baadaye wamshauri ipasavyo ili kumsaidia baadhi ya utaalamu wa pale, kwa hivyo, watakwenda huko. Tunakusudia katika Bajeti yetu kila mwaka tutaanza kutenga fedha maalum kwa ajili ya kuandaa Skuli ya Sekondari ya Kengeja kwa ajili ya masomo ya sasa hivi na ya baadaye. Suala hilo tutaliangalia kwa makini sana ni pamoja na kuongeza baadhi ya madarasa pale na *Workshop* za pale ili ziweze kukidhi mahitaji yaliyokusudiwa.

Suala la kwamba Mhe. Muhunzi aliposema ni vyema taasisi kama hii ikawa na *annex* yake, ikawa na *branch* yake kule Pemba. Mimi nasema hilo sio lazima sana, kwa sababu tukisema hivyo kutakuwa na mambo mengi ambayo yatatukwaza huko mbele, kila tunachofanya upande mmoja na upande wa pili tukifanye. Kuna mengine tunayo uwezo nayo tutayafanya, lakini yale ambayo hatuna uwezo nayo tunahisi kwamba itapunguza gharama basi tutafanya hivyo.

Mhe. Spika, Mhe. Omar Ali Jadi nataka nimtoe wasi wasi kuhusiana na kile Chuo cha Uwalimu tulichokiahidi, nataka utulie kabisa wala usiwe na mashaka. Chuo kile tumekitengea kutokana na pesa ambazo tumezipata kutoka Benki ya dunia karibu bilioni 2 yaani dola *one point five million* (1.5 milioni) kitajengwa Mchanga Mdogo.

Taratibu za kumtafuta mshauri wa ujenzi ndio zinaendelea karibu tuta *shot list* baadaye na tutatafuta utaratibu wa kupata wakandarasi. Mheshimiwa nakuhakikishia kabla ya mwaka 2010 haujamaliza muda wako, basi Ishaallah kazi hii ya chuo utaiyona pale na tutakuwa pamoja katika kuhakikisha shughuli zinakwenda vizuri, chuo kipo. Lakini hatuwezi kusema kwamba tunajenga chuo kile Mchanga Mdogo, basi tutafute na chuo kingine hapa Unguja. Hilo halitowezekana kwa sasa hivi. Huko mbele tutakuja kuangalia hali itakavyokuwa inaruhusu.

Kwa mfano kuna masomo ya biashara yapo Dodoma sasa hatuwezi kuwaambia watu wa Dodoma jamani tujengeeni na chuo kimoja Unguja kule tunapata shida. Masuala haya yana mahali pake, kuna masomo mengine huyapati hapa ndani ya nchi ya Tanzania unayapata nje ya nchi.

Mhe. Spika, Chuo cha Karume kipo kimoja tunakiimarisha hiki na kuwapa fursa kwa wale ambao watatoka Pemba vile vile kupata nafasi ya kuja kusoma Chuo cha Karume kama ambavyo tunafanya sasa hivi na tutaendelea kufanya hivyo.

Mhe. Spika, kuhusu ubovu wa majengo tumesema siku nyingi na bado tunaendelea. Tatizo lililokuwepo ni urasimu wa benki ya dunia, kwa kweli hata mimi unanikera, isipokuwa sina la kufanya. Nitafanyaje ndio wenyewe wameshapanga. Jambo la kulitekeleza kwa miaka miwili mitatu wao wanachukua kama miaka kumi maana yake sio kama miaka kumi, lakini ni mara mbili zaidi. Mara apatikane huyu mara apatikane huyu.

Mimi husema kwani pesa tumeshaambiwa na tumeshazipata hizi hapa sasa tunasubiri nini. Kwanza mshauri wameweka miezi sita lazima ikamilike, akisha mshauri atafutwe mchoraji achore miezi sita.

Mimi mawazo yangu nilikuwa nawambia hata wale watendaji kwani ni lazima tusubiri kipindi hicho na hata ukirahisisha kwamba wapeleke Benki ya Dunia wanakwambia bado wacha twende kwa utaratibu. Kwa hivyo, mwaka huu wa 2009 utakuwa kwenye matayarisho ya kutafuta wakandarasi na mambo mengine. Tunatarajia kazi nyingi zitaanza 2010 tukijaaliwa.

Kwa hivyo kuhusu Chuo cha Fidel-Casro, Utaani, Uweleni zote hizi Mwenyezi Mungu akipenda kabla ya mwaka 2010, hatujamaliza muda wetu humu ndani ya Baraza tutashuhudia kunafanyika marekebisho makubwa. Gharama zake ni sawa kama zinajengwa upya. Pamoja na juhudi zilizochukuliwa za kujenga jengo la ghorofa na hatukusudii lile kuliondosha, bali tutaliimarisha zaidi. Lakini yale mengine ya zamani yote tutayaondoa na tutajenga upya. Mwenyezi Mungu akipenda tutakuja kukumbuka kwamba haya ninayosema kwamba siku moja Mwalim Haroun alisimama pale mbele ya Baraza na akatuahidi, tutayaona matunda yake Ishaalla na vifaa vyote muhimu vya sayansi na kompyuta vitakuwepo katika maskuli hayo tunayoyatengeneza.

Mhe. Spika, ubovu ni ubovu na ukishakufika umri tena basi. Mhe. Abassi Juma Muhunzi nadhani hapa yupo na Mhe. Kamal bahati mbaya hayupo, hawa walikuwa ni wachezaji mpira mahiri siku za nyuma. Tulikuwa tunafanya mazoezi hapo Mau, basi humwambia Mhe. Kamal na Mhe. Muhunzi tia mpira pasi na mimi nipate kufunga goli na kweli ningefunga, basi anazunguruka sio kama anataka lakini mwili hautaki, hata aliponitilia mpira pasi, wapi . Kumbe anajitayarisha ili anyanyue mguu, ananambia mguu ulikuwa haunyanyuki , sio makosa yake simlaumu ndio umri unavyokwenda. Sasa na majengo haya ya Karume kweli hayawezi kuwa kama yalivyokuwa miaka ile ya 60 na 70. Mhe. Kamal Basha bahati nzuri anaingia. (*Vicheko*).

Mimi nikikuonyesheni picha yangu niliyopiga miaka ya 70 nilipokuwa nacheza mpira hizi nywele nilizokuwanazo hivi sasa hamna kitu, lakini wakati huo zilikuwa zinafika mpaka mabegani, hujitizama kwenye ile picha na nikajitizama na sasa hivi, sitoki machozi, lakini nitafanyaje ndio wakati na sote ndio tunakotoka. (*Vicheko*).

Kwa hivyo na haya majengo ya Mbweni ilifika mahali yakawa hayana maana pesa mbili. Wakaja wenzetu wa danida wakafanya ukarabati Mbweni, wakafanya Skuli za Sekondari zote za Unguja, wakafanya all most Skuli zote za Pemba. Ndio yale mabati mekundu ambayo tunayaona. Tumetumia kwa muda mrefu mpaka leo yamerudi katika hali ile. Sasa tukiweka Taasisi hii ya Karume pale kuwapa nguvu na watakuwa na uwezo wa kutafuta fedha zao na watapata bajeti yao serikalini bila ya matatizo yoyote. Mimi nina imani kabisa kwamba hilo litawezekana.

Hivi juzi au pengine jana tumeshuhudia kama tumetizama vyombo vya habari, Katibu Mkuu amekwenda kuzindua mradi au *Workshop* itakayojengwa kwa msaada wa Wajerumani. Wanamakubaliano na Chuo cha Karume na wametuahidi baada ya mwaka mmoja itakuwa tayari, *Workshop* ya mambo ya magari. Gari zetu hivi sasa za a*utomatic* tunazotumia inatubidi fundi ni lazima atoke Dar-es-Salaam au atoke sehemu nyengine, sasa ile *Workshop*

itakayokuwepo pale itatuwezesha magari yetu haya kutengenezwa pale pale. Mimi naona ni vyema kwamba serikali tukashauriana zaidi. Hata haya magari ya viongozi na wengineo basi yakafanyiwe *service* pale pale, ili tukiimarishe zaidi Chuo chetu cha Karume na uwezo wanao. Vijana wale wana uwezo mkubwa kweli wa kututengenezea magari yetu. Nina hakika tukiwapa nguvu, basi mambo yatakwenda vizuri. *Workshop* ile baada ya miaka mitano wanakabidhiwa Chuo cha Karume kinakuwa chini ya uongozi wao. Hivi sasa tutashirikiana na Wajerumani na Wakorea wapo pale tunashirikiana nao.

Mhe. Spika, nilizungumza kuhusu jina likatia mashaka kwamba hili sayansi na teknolojia kuwekwa pamoja. Sisi Wizara ya Elimu hatuwezi kuibagua sayansi kwenye masomo haya. Hii teknolojia inatokana na masomo ya sayansi mbali mbali, uta- *apply physics* ndani yake, *mathematics* maana sayansi tusikusudie kwamba ni *Chemistry* na *Biology*, *physics*. Hii sayansi itakuwa ndani ya masomo ya kiutalamu ya kiufundi yatasomeshwa masomo hayo, na isiwe tatizo sana la jina. Kwa hivyo, *institute* itabakia kama ilivyo. Pamoja na ushauri tuliopewa tunaomba kwamba bado iendelee na ijulikane kwa jina hilo hilo kwa *Institute of Science and Technology* ya Karume.

Halafu kulikuwa na suala zima la kuona kwamba hili suala la *technical education* kama lina mafunzo ya uwalimu, nitatoa kwa ujumla kwanza halafu kama wasaa utakuwepo nitajaribu kutoa mmoja mmoja. Labda watu walifikiria kwamba tuna *component* ya mambo ya mafunzo ya uwalimu. Hii ni elimu ya ufundi na walimu wake wamefunzwa kusomesha masomo haya ya kiufundi, *training* yao waliyoipata ni hii ya *technicala education*.

Kwa ujumla masomo ya taaluma za ufundi wa aina mbali mbali hujulikana kama ni *technical* and *vocational education* na hakuna mahusiano yoyote ya mafunzo ya uwalimu. Suala hili linamwezesha mtu kujiandaa vizuri katika *level* mbali mbali ambazo tumezitaja na kuweza kujisomesha pale pale bila ya kwenda kwengineko. Akimaliza *level* ya 1, anaingia *level* ya 2, anaingia ya 3, anaingia ya 4, ya 5, ya 6 mpaka anamaliza level ya 10 atakuwa keshapata PhD pale pale Chuo cha Karume na Mungu akijaalia Ishaalla hilo litawezekana.

Mhe. Spika, kuhusu masuala ya kufutwa Taasisi mbali mbali limejitokeza na kusemwa kwamba Nkuruma tumeifuta na Taasisi ya Kiswahili tumeifuta. Mheshimiwa Taasisi ya Kiswahili ipo. Katika hesabu kuna kitu kinaitwa *universal set* ndani yake kuna kitu kinaitwa *sub set*, sasa Taasisi ni *sub set* ya SUZA ile inakuwa ndio kama *universal* set na ipo pale na zinatolewa Stashahada hapo hapo Taasisi ya Kiswahili. Nkuruma nayo pia haikufa nayo pia ni sehemu ya SUZA kwa hivyo nayo pia ipo. Ilikuwa inatoa *certificate* sasa hivi haitotoa *certificate* isipokuwa SUZA ndio itatoa *certificate*, kama itatoa

diploma basi itatoa diploma ya *umbrella* iliyokuwa chini ya SUZA. Kwa hivyo vile vyuo vipo na havijafa na tusingefurahi hata sisi kwamba viondoke.

Hivi sasa tunaanza kuzingatia tuna Chuo cha Benjamin Mkapa kule Wete, tutapojenga chuo hiki kwa Mhe. Omar Ali Jadi. Akauliza je, tukiite bado Benjamin Mkapa au tukiite Mchangamdogo *Teachers Training College*. Hilo tutaliangalia. Lakini tunaweza tukatafuta taasisi nyengine ikakidhi haja ya pale mahali. Kwa hivyo haya majina yatakuwepo na hatukuliondosha jina hili la Nkuruma kutokana na kwamba tunaliheshimu na tutaendelea kulienzi.

Mhe. Spika, masomo ya Sayansi uimarishaji wake. Hivi karibuni nilisema mahali kwamba Uingereza wana upungufu wa walimu wa kusomesha *Physics*, wao wana walimu elfu saba. Mimi nikipata walimu 70 tu wa *Physics*, basi watanifanyia kazi nzuri sana. Wenzetu walimu elfu saba wenzetu wanaona ni upungufu. Hapa nayasema mimi lakini huko yalisemwa na wenyewe mawaziri. Masomo ya sayansi na hesabu dunia nzima ni kero.

Marekani wanasema hilo hilo. Wale wanafunzi wetu wawili wanaosoma Marekani, kuna kijana yule anaiitwa Daudi kaondoka kule anachukua *Mathmatics* katika *State University* Carolina. Hivi sasa wanamtumia katika *institute* mbali mbali anakwenda kufundisha kwa sababu na wao hawana mtaalamu. Kijana wa Kizanzibari ameweza sasa hivi kuwa kule ndio hazina kubwa Marekani na Mwenyezi Mungu amemjaalia yule kijana ana kipaji sana. Anasomesha na anakwenda kwenye mihadhara mbali mbali kwa somo la hesabu. Na yule mtoto mwanamke kwenye Biology anafanya hayo hayo. Kwa kweli matatizo ya hesabu yapo na ya biology yapo na ndio maana tukaanzisha *dipertment* ya *science* hapa SUZA. Tunashukuru Chuo cha Chukwani kinasomesha masomo hayo ya Phiysics na Mathematics.

Chuo cha SUZA tulikitaka kianzishe diploma ya sayansi na kamati ilipokwenda wameambiwa kwamba hakuna pesa za kuweza kuanzisha *department* ya sayansi. Wakati mwengine hatutakiwi kutoa siri za nyumbani. Kamati iliwaeleza kwamba haya ni matatizo ya *administration* yao wenyewe SUZA. Kwani ile Diploma ya Sayansi iliyokuwa ikitolewa Nkuruma chini ya udhamini wa Wizara ya Elimu tulikuwa hatuwapi pesa.

Wengi humu tumo tuliofaidika na diploma ya sayansi pale. Lakini tulianzisha katika hali hiyo hiyo mwaka 1979, benchi ya kwanza ilijiunga na diploma pale, mimi niliingia benchi ya pili mwaka 1980, kwa hivyo kukawa na ya *language*, pakawa na *social scienci* na *physics*, *mathematics*, wapo waliopata diploma, tena mtihani ule haufanywi kama unaotungwa na maalim Haroun ni Baraza la Mitihani ni *standard* kabisa na Alhamdulillah walimu wetu wengi walipitia pale.

Sasa SUZA wanaposema hawana pesa hayo ni matatizo yao ya *management* ya ndani. Lakini mimi ile *concern* niliichukua siku ile waliponieleza na tunalifanyia kazi na tutanatarajia wataanzisha *anytime*. Hakuna sababu ya kwamba kozi ile kwa nini isianzishwe. Tuliwapa jukumu la kuanzisha kozi ile lakini pia tumewapa jukumu la kuanzisha kozi ya *management* ya uongozi na hilo nalo vile vile tutahahakikisha nalo linaimarishwa.

Tunachukua juhudi na njia mbali mbali ya kuwasaidia ili waweze kuanzisha kozi hizo. Sababu ya kwamba SUZA haijaanza diploma ya sayansi kwa ukosefu wa pesa hilo sio la msingi wowote ni matatizo yetu ambayo tunayachukua na tutakwenda kuyafanyia kazi kuona kwamba jambo hilo halicheleweshi zaidi.

Imebidi tulazimike kuzilazimisha taasisi zetu za Chuo cha Kiislamu na Kiuyu Micheweni kuanzisha programu za diploma. *Certificate courses* tumeziondosha na tumeziondosha kwa nia nzuri tu. Kwa mujibu wa *ratio* walimu wa *primary* ni wengi lakini kuna maeneo tunajua kuna *shortage*, wanahitajika hata hao walimu wa *certificate*, lakini badala yake tukapandishia hadhi tukasema tuanzishe diploma ya msingi na sasa hivi tunashukuru kwamba tunao wanafunzi wengi tu wanachukua diploma ya msingi katika vyuo vyetu vya ualimu.

Vile vile diploma za *science* matatizo hayo yanaweza kutuchukua miaka miwili mpaka mitatu, baada ya hapo nina hakika pamoja na kwamba wizara inaendelea tutahitaji zaidi matatizo yetu ya walimu yatapungua kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hivyo, tunakiri kwamba kuna ukosefu wa walimu wa *science*, lakini Mwenyezi Mungu akipenda katika programu zetu na Benki ya Dunia, *USAID* tumeshirikiana vizuri tutaandaa walimu na programu maalum za *science* kuweza kutufikisha pahala pazuri.

Mhe. Spika, ushauri mwengine uliotoka hapa, si ushauri ni pendekezo kwamba kulikuwa na tatizo linaonekana labda la uteuzi wa wajumbe. Nasema kama nilivyosema nazungumza kwanza kwa ujumla halafu nitakwenda kwa mmoja mmoja kama wakati ukiniruhusu. Ile *version* ya Kingereza ni sahihi zaidi kuliko ile ya Kiswahili, tafsiri kidogo ilitucheza. Kwa sababu wajumbe wote waliowekwa pale ukitizama ni tofauti na kwenye Kiswahili, Kishwahili wanaonekana watano halafu baada ya hao kuna na watatu wengine.

Kwa hivyo, inaelekea wajumbe watakaokuwepo pale sio watano watakuwa ni wanane, lakini pale katika wale watano, waziri anashauriana na zile taasisi tano zinazohusika pale halafu anateuwa na wengine watatu kwa mujibu wa sheria yetu inavyotueleza. Kwa hivyo, wajumbe wote pale watakuwa ni wanane naomba hilo lifahamike, ile tafsiri ya Kiswahili ilikuwa na matatizo mengi

kama wenyewe Wajumbe walivyosema. Vile vile kulijitokeza tatizo la maana hata kuweza kuitafsiri ile ya Kiingereza ukiitizama inaonekana iko wazi moja kwa moja wala haina matatizo yoyote.

Mhe. Spika, naomba sasa uniruhusu kwa kiasi fulani niende kwa mtu mmoja mmoja haraka haraka ili nikamilishe ile saa yangu niliyokuomba. Mengine ambayo nimeshayatolea ufafanuzi, basi itakuwa ndio nimeshayatolea hatuna haja ya kuyarejea rejea.

Mhe. Spika, watu walizungumzia hofu ya viwango vya cheti pengine na mitihani ya pale chuoni. Napenda niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba mitihani pale itasimamiwa na taasisi inayoitwa *NACTE*. Hii ni Taasisi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyeti vinavyotolewa pale, vile vile vitasimamiwa na taasisi hiyo. Napenda nikutoeni hofu kwa sababu wengi waliingia hofu, kidogo kidogo tutakwenda siku itafika, kwa sababu masuala ya elimu ya juu ni masuala ya Muungano. Kinadharia inaona kweli ni hivyo na katiba yetu imesema.

Mhe. Zakiya Omar Juma ali-*quote* leo asubuhi kwamba kipengele nambari 14 kimeingizwa pale kuwa ni suala la Muungano. Ni kweli ni suala la Muungano, lakini mpaka hivi sasa ninavyozungumza mimi bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar haijawahi kupokea au kupata hata shilingi moja kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika ku-*supplement budget* yetu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa inachukua mamlaka kamili yenyewe ya kuisimamia wizara yake katika bajeti yake ya elimu ya juu, *SUZA* iko hapo.

Tunapopeleka vijana wetu hata kama ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam au popote pale Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndio inayoshughulikia masuala hayo na tutaendelea na hiki Chuo cha Karume ni chetu na *Inshaallah* kitaendelea kuwa ni chetu, tutahakikisha kwamba mafunzo yale yote tunayasimamia wenyewe.

Leo hii tuna taasisi za vyuo vikuu vitatu, Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka wameshapata ithibati katika ile taasisi yenyewe kuanzia miaka miwili baadae pale itatoka *degree* ya uongozi wa fedha, kitakuwa ni chuo cha nne kutoa *degree* hapa Zanzibar chetu wenyewe kinamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Chuo cha Karume kitakuwa ni chetu wenyewe na kitakuwa ni chuo cha tano na vitaendelea na vyengine. Chuo cha Kiislamu tukijaaliwa tumo katika mipango hiyo hiyo *degree* ya Kiislamu na masomo ya Kiarabu yatolewe hapa hapa Zanzibar Mazizini na kule Micheweni Kiuyu tutoe *degree* mbili na uwezo huo

tunao. Wasomi wa Dini ya Kiislamu wenye *masters* ni wengi na hivi sasa kuna kama walimu wetu wawili, watatu wako nje wanachukua mafunzo ya *PhD* tunawasubiri wakirudi tu, tuanzishe utaratibu wa kuanzisha Vyuo Vikuu vya Kiislamu hapa Zanzibar na Mwenyezi Mungu atatujaalia hilo litawezekana.

Kwa hivyo, ni kweli ya Muungano, katika Muungano kuna Mfuko wa *Tanzania Education Authority* wanatusaidia. Chuo cha Karume kimesaidiwa nadhani kimepata kama milioni mia moja, *SUZA* na wao walisaidiwa kwa kiasi fulani, lakini hii misaada inakwenda kwenye *individual institution* sio kwamba inakuja serikalini moja kwa moja. Elimu ya juu bado inaendelea kusimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, tunaomba sana tuendelee kukiunga mkono au kuiunga mkono serikali katika suala zima la kukiimarisha chuo chetu hiki cha Karume na tusiwe na mashaka. Mwenyezi Mungu akipenda *Inshaallah* yote hayo yatatengenea.

Mhe. Said Ali Mbarouk alikuwa na mengi sana mengine nimeshayajibu na alipendekeza suala moja kwamba huyu waziri kwa nini asiitwe mwenye dhamana anayeshughulikia sayansi na teknolojia? Kwa sababu huko mbele pengine tutakuwa na wizara ya sayansi na teknolojia, lakini unaposema waziri wa elimu, elimu imekusanya sayansi na teknolojia. Kwa hivyo, hakutokuwa na haja kubagua kwa kusema kwamba kwa wakati huu hatujui huko mbele, lakini kwa wakati huu madhali tunayo wizara moja tu ya elimu ambayo inashughulikia mambo yote kuanzia elimu ya maandalizi mpaka elimu ya juu tuendelee kukubali kwamba basi hapa akitajwa waziri awe ni waziri yule anayeshughulika na mambo ya elimu.

Kwa mfano, sasa hivi masuala ya *UNESCO* wenzetu wa Tanzania Bara Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi sisi tunasema Mafunzo ya Amali ndio hayo hayo, ufundi na amali ndio hayo hayo masuala ya kazi, amali ni neno la Kiarabu. Masuala ya *UNESCO* yote yapo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, masuala ya sayansi yamepelekwa Mawasiliano nadhani kuna wizara kama hiyo.

Masuala ya *UNESCO* ambayo ndani yake kuna utamaduni, elimu, sayansi yote yameachwa pale pale kwenye Wizara ya Elimu na Ufundi na bado waziri yule ndiye dhamana kwa kule, Prof. Jumanne Maghembe na kwa hapa Zanzibar kwa wakati huu mpaka sasa hivi ni Maalim Haroun Suleiman ndiye anayeshughulikia masuala hayo kwa niaba ya serikali. Kwa hivyo, naomba hilo tulikubali.

Pili suala la mwenyekiti kwamba hakuwekewa sifa. Hili mara nyingi huwa linajitokeza, bahati nzuri mwenyewe alijibu akasema najua nitaambiwa kwamba rais asiwekewe masharti haya na tumwachie mwenyewe, tusimwekee hayo masharti tutamshauri na yeye mwenyewe anao uwezo huo wa kuweza kutafuta watu kama hao. Mabaraza yetu mbali mbali wanachagua watu madhubuti sana na mambo yanakwenda vizuri. Kwa hivyo, na hii nafikiri Mhe. Rais wetu atatuchagulia mtu muwafaka kabisa.

Sasa tukimuwekea kwamba lazima awe na *degree* unajua wakati mwengine tusifikiri *degree* ya kwanza, ya pili na ya tatu ndio mtu anakuwa *administrator* mzuri sana au akawa mtaalamu mkubwa sana. Pale Skuli ya Mikunguni kuna Mzee mmoja kwa wale waliokuwa walimu watamkumbuka kama sikosei jina lake anaitwa Mzee Yahya, ni kapenta anachonga milango. Alipokuja Rais Mstaafu wa Nigeria alitembezwa pale akaona mlango mkubwa akauliza kafanya nani? Akaambiwa huyu hapa ndiye aliyefanya, akasema aniletee mlango aje anifungie Nigeria. Lilinunuliwa lango sijui milioni ngapi kalitengeneza yule babu akenda akamfungia Nigeria hata chumba cha tatu hakufika.

Kule India siku moja nilikuwa nasikiliza hadithi moja inasema hivi: ”Alikuja mtaalamu mmoja kutengeneza reli pale Bara akaambiwa tupe vyeti vyako. Akasema *in India paper not important, brain is important”.* Anasema *paper* si muhimu, muhimu *brain*. Sasa yule mzee anasema hana cheti cha *PhD,* lakini mlango akikufanyia *curving* zake zimeshindwa hata hizo mashine zinazotumia *degree*. Kwa hivyo, inawezekana tukampata mtu akawa hana *degree,* lakini akawa na busara na hekima akaweza kufanya kazi vizuri kweli kweli na mimi naamini hivyo. Kuongoza jambo sio lazima uwe na *degree*, kubwa ukiwa na busara na hekima zako utafika vizuri. Sisi humu wengi hatuna *PhD,* lakini *Alhamdulillah* majimboni huko mambo mazuri na *Inshaallah* yataendela kuwa mazuri.

Mhe. Spika, Mhe. Said Ali Mbarouk aliuliza sana tumejitayarisha? Kwa sababu huko chini kubovu, lakini mimi sikumfahamu sana atanisaidia baadae. Anasema chini kubovu mimi nimemfahamu kwamba labda huko kwenye skuli za msingi, za sekondari ana wasi wasi nako. Sasa napenda nimhakikishie kwamba kuanzia elimu ya maandalizi, msingi na sekondari hapa matayarisho yake yamekaa vizuri sana, vitabu tunavyo vya kutosha.

Leo hii naomba nitoe taarifa Mhe. Spika, vile kitabu cha *phyisics* cha *Form I* mpaka *Form IV* tayari vimeshaletwa wizarani na Mwenyezi Mungu akipenda vitasambazwa. Kwa hivyo, sasa hivi kuanzia *Form I* mpaka *Form IV* vitabu vyote vya sayansi vitakuwepo mashuleni na watoto watapewa kila mmoja atachukua nyumbani asiuziwe bure, akipoteza atalipa. *Form V* na *Form VI*

Chemistry, tayari vimeshakuja, *Physics* na *Biology* na hesabu vitapatikana tukijaaliwa ikifika kati kati ya mwaka huu tunatarajia watu wetu wa *Form I* mpaka *Form VI* wote watakuwa na vitabu.

Jana nimesikitishwa sana na kitendo kinachofanywa na baadhi ya watu ambacho si kizuri, wameanza kuvichukua vitabu vyetu vimeandikwa hivi ni mali ya serikali ambavyo ndio Zanzibar visiuzwe viko madukani na watu wanaviuza. Sasa hivi vyombo vinavyohusika tunavijulisha kama vinasikia ndio wakafanye hiyo kazi na vinauzwa katika maduka mbali mbali.

Vitabu hivyo vimeandikwa hasa mali ya serikali haviuzwi na kwa Kizungu vimeandikwa *not for sale*, sasa kama mtu kaona *not for sale* labda kaona cha mwalimu sale aa, itakuwa makosa hayo, lakini kimeandikwa kisiuzwe. Sasa naomba sana hilo suala limenisikitisha na naomba tusaidiane kwa sababu tunaokwenda kuwanunulia watoto wetu ni sisi na vitabu vile vimeandikwa vya SMZ cha Kingereza darasa la nne na cha Kiswahili darasa la nne. Sasa kama vimetolewa kwenye ghala yetu, kama vimetolewa skuli vimepelekwa au pengine hao *publishers* wetu wameanza kuviuza hilo tutalifuatilia, nilitaka nitoe taarifa hiyo ijulikane.

Mhe. Spika, kwa hivyo, chini huku kwenye msingi nilivyofahamu na sekondari na kwenye vyuo vyetu hivi pamoja na taasisi za Karume, Mikunguni na Kengeja tutajitahidi kuimarisha zaidi na ninakuhakikishieni Waheshimiwa kwamba hili suala litakaa sawa tukijaaliwa. Jambo lolote utapata mitihani, lakini hatimaye utafika mahali ulipokusudia.

Mhe. Spika, nimesema kwamba wajumbe wangekwenda Karume, nimemwambia Mwalimu Mkuu leo hii hebu niletee zana kweli unazo za kutosha? Naomba niyasome hayo niliyoletewa katika Chuo cha Karume na Mwalimu Mkuu wa pale hanidanganyi. Anasema hivi:-

”Mradi wa *Video Comference* ambao umehusisha taasisi nne hapa Zanzibar *SUZA, ZIFA, Karume Technical College* na *ZU* kila taasisi imepata *video comference equipment* moja na *smart board* kwa ajili ya kusomeshea. Hii ni sehemu ya pili baada ya ule wa mwanzo wa kusambaza kompyuta ambao uligharimu karibu dola laki mbili na hamsini. Chuo cha Karume hivi sasa kuna kompyuta 72 madogo hayo jamani Waheshimiwa Wajumbe? Zana za kisasa pia zipo pale tuondoshe mashaka.

Mimi nasema vifaa vipo, zana zipo isipokuwa nataka nikuhakikishieni kwamba hatutoanza leo na kesho, tutakwenda nalo kidogo kidogo kama walivyotushauri wenzetu pengine inawezekana tusianze mwaka huu. Sera ya Elimu inasema elimu ya maandalizi ni ya lazima, lakini utaona mpaka leo hatujaweza kuanza

elimu ya maandalizi tukasisitiza kwamba lazima watu wapitie elimu ya maandalizi, isipokuwa tumeliondosha lile darasa moja tu la *OAC* wengi tulikuwa tunaliita *Form One Zero*.

Tumeliondosha kwa sababu halina haja ya kuwepo pale, miaka 15 mpaka 18 limekuwepo pale tukasema tulipunguze matokeo yake wanafunzi wote waliokuwa *OAC* na waliokuwa darasa la saba wote tukawapeleka *Form I* mwaka huu wamefika *Form II*. Idadi ya wanafunzi waliofanya mtihani wa *Form II* safari hii ni mara mbili zaidi, kulikuwa na vijana karibu 42,000 wamefanya mtihani huo wanangoja matokeo ambayo tukijaaliwa mapema mwezi wa February tutayatangaza.

Nina hakika tutapata vijana wengi sana waliofaulu, nina hakika kabisa, lakini tulifumba macho tukasema hapa tuamue hili na tumeamua na limewezekana. Kwa hivyo, sasa hivi mwanafunzi akifika darasa la saba anaingia *Form I*, lakini sisi sera inatwambia akifika darasa la sita basi aingie *Form I*, hata hilo hatukuliharakisha mpaka tuhakikishe tuna madarasa ya kutosha ya sekondari. Tunangojea Benki ya Dunia yatapoanza kuenea katika kila wilaya, tutafika darasa la sita tutawasambaza katika skuli zetu za sekondari, tutawatizama na huko mbele miaka mitatu mpaka minne ijayo kwa upande wa maandalizi. Mimi nina hakika Mwenyezi Mungu atatujaalia hasa kwa nguvu ninazoziona kwa wananchi katika ujenzi wa madarasa.

Kuna madarasa zaidi ya 1,653 sasa hivi yanayongojea kukamilishwa na serikali, kila unapopita unakuta *extention* ya madarasa. Naomba nichukue nafasi hii Mhe. Spika, kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako wote kwa kweli wanajitahidi sana katika kusimamia maendeleo hayo na naomba waendelee.

Kwa hivyo, tusiwe na mashaka juu ya vifaa, walimu, majengo ndio kama nilivyosema sina haja ya kurejea tena. Lakini *degree* nzuri hutolewa pale penye walimu na vifaa vinavyofaa si lazima kwenye jengo ambalo ni jipya, lakini likiwa jipya linapendeza kama WEMA Mazizini pale *Alhamdulillah* panapendeza sana sihaba, ukienda Pemba Chake Chake pale utaliona jengo jipya la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali linapendeza na tutazidi kuliimarisha kwa kuweka vikalio na *furniture* mpya mle ndani ili liwe zuri zaidi *Inshaallah*. Kwa hivyo, nia ni nzuri na tutajitahidi kuendeleza.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Suleiman Ali yeye kafika mbali alikwenda India, Mhe. Said Ali Mbarouk akenda Pakistan akamtafuta Mzee Bhuto alipo pale kwenye *Research Institute* ile na mambo mengine. Tumekuelewa na tusiwe na hofu kama nilivyokwisha kusema kwamba madhali nia ni nzuri, basi mambo yote yatakwenda na wewe mwenyewe ulisema kuwa ni *product* wa pale Karume. Mimi nakushauri Mheshimiwa utapokuwa na nafasi wewe nenda kakae na

uongozi wa chuo uwashauri tutashukuru sana, wanasema ni ushauri wa bure unaotolewa. Kwa hivyo, uende pale unapoona unaweza kuwasaidia uwasaidie.

Mhe. Hamad Masoud karibu alizungumzia yale yale ambayo Mhe. Said Ali Mbarouk na wengine waliyazungumza, akatoa mfano wa miaka 60 yeye alipo-*graduate* pale. Tena jamani turudie yale yale tu, ya zamani ndio ya zamani, kweli walisoma pale, lakini walikuwa wangapi? Waliposoma wao walikuwa hawazidi wanafunzi 50 na utaratibu wa kuingia pale zamani ukitoka *Form I* au *Form II* unaingia pale mwaka wa mwanzo wanaita *senior one*, *senior two*, *junior*, kulikuwa na level kama hizo. Ilikuwa wakipasi moja kwa moja wengine badala ya kwenda *Form III* wanaingia pale mwaka wa kwanza, wa pili wanasoma miaka mitatu wakifaulu wanaendelea, lakini baadae utaratibu ule ukabadilika na mabadiliko ya maendeleo ya nchi vile vile yanatubadilisha.

Zamani ilikuwa mwisho kufika darasa la sita, la nne, tumefika darasa la saba tukenda la nane, tukarudi tena la saba, sasa hivi tumeshaweka sera mpya kwamba mwisho darasa la kumi na mbili. Huko miaka 30 ijayo watakuja wengine watasema hapana turejeshe utaratibu mwengine, lakini sisi tulipeleka darasa la kumi na mbili kwa maana gani? Kwa Bara kule wenzetu wana tatizo kubwa zaidi kwa sababu wao wakifika darasa la saba hawaendelei na masomo basi, *population* kubwa inakuwa nje bado watoto ni wadogo wanapata matatizo, *brain* hazija-*mature*. Lakini hawa wa kwetu hapa wakimaliza darasa la kumi pia tumehisi bado akili zao hazija-*mature* ndio maana yake sera ya Wizara ya Elimu ikasema amalize darasa la kumi na mbili na mtoto akifika *Form II* kwa kiasi fulani anao uwezo.

Kuna mmoja alisema watoto wetu wanafeli Kiswahili. Uingereza wanafeli Kingereza, Waingereza wale Wazungu kwenye mitihani ya Kingereza walisema hivi juzi kwenye magazeti na mitandao mkitizama mtaona somo la *English* Waingereza wenyewe wanafeli. Kwa sababu masomo ni tafauti na lugha yako mwenyewe, sasa hao wanaofeli Kiswahili sio kwa sababu hawakijui Kiswahili mtihani ni mtihani jamani, kwani yule Imam anaposalisha *kul-ya* anakuwa haijui? Lakini pale yupo mbele *kul-yaayuha lkafiruun* anakwenda akirudia yale yale tu, mpaka anasema *Allahu Akbar* anaona hayeshi. Sio kwamba ile sura haijui na huku nyuma utasikia kuna watu wanatoa kauli ya kumwambia kwamba kuna kitu hapo anasimama akirudia pale pale. Sasa mimi nasema kufeli kwa Kiswahili tusione tatizo, au tunasema kiwango chetu cha elimu kiko chini kwa sababu mtoto hawezi kusoma Kingereza. *(Kicheko)*

Juzi tulipokuwa Nungwi wananchi wa Nungwi walilalamika wanasema wananchi wetu hawapati kazi kwenye mahoteli kwa sababu watoto hawajui kusema Kiingereza wanavyoambiwa. Wakaambiwa kwani kule China anayetandika kitanda anazungumza Kizungu? Na wewe kama unataka useme

Kizungu kwa madhumuni gani unayotaka kuzungumza naye yule? Wewe mwenye hoteli kwamba mfanyakazi wako lazima unataka ajue Kizungu unataka nini? Wewe kazi yake ushamwambia akatandike kitanda sasa hakitaki Kizungu. Kwa hivyo, mambo kama hayo. Mimi nasema tusi-*generalize* sana na tukatoa *quick answers* kwenye masuala kama haya.

Masuala ya elimu na ubora wa elimu ni mambo ambayo yanahitaji mjadala mrefu, wala tusiamini kwamba watoto wetu hawawezi kusoma magazeti kwa Kingereza ndio hawana elimu sio. Mitihani yote ya *Form IV, Form V, Form VI* ukiacha Kiswahili iko kwa Kingereza na watoto hao wanapasi, wanapata *first division, second division, third division* na *fourth devision* na wale wachache wanapata ziro kwa bahati mbaya. Lakini wanapasi na lugha wanayotumia ni hiyo ya Kingereza. Kwa hivyo, haya masuala tuyaangalieni kwa upana zaidi.

Mhe. Spika, tunahakikisha tutaendelea na ninamuomba Mhe. Hamad Masoud pale aliposema tungerejesha hali kama ile angeunga mkono kwa asimia mia mbili, bahati mbaya hayupo, lakini namuomba aunge mkono kwa asilimia mia moja tu inatosha hakuna haja ya asilimia mia mbili. Tafsiri ya Sayansi na Teknolojia nimeshaitoa sina haja ya kuirejea.

Kumezungumzwa kwamba hali ya Chuo cha Karume ni mbaya sana. Unajua mpaka mnanitisha hata mimi, unaposema hali ya Chuo cha Karume ni mbaya sana mimi ilibidi nifanye safari niende nikachungulie hiyo hali mbaya, matatizo madogo madogo nimesema hayakosi, lakini jamani chuo hicho hakiko katika hali mbaya. Bado Mhe. Spika, nasisitiza, naomba Wajumbe wako ikiwezekana hata wote wafanye utaratibu wakatembee Chuo cha Karume na Mkuu wa Chuo nina hakika atawapatia japo kuwa soda kidogo na chochote cha kutafunia wakakione. Kwa sababu kuona si kusikia, huyu waziri anayetwambia haya maneno anatwambia kuna makompyuta, vifaa ni kweli? Mimi naomba waende na wataviona vifaa hivyo na hao wataalamu wako watawakuta pale.

Masuala ya uteuzi nimeshayatolea ufafanuzi sina haja ya kurejea tena. Majengo ya Nkrumah nimeshayatolea ufafanuzi bado yapo na yanaendelea. Kweli tunahitaji kuwa na majengo mazuri.

Mhe. Rashid Seif nakushukuru sana na kama ulivyosema kwamba kwa mara ya kwanza unamshukuru rafiki yako kwa kuona *library* pale, lakini bado inapwaya kwa sababu vitabu havijawa vingi na bahati nzuri juzi alikuja rafiki yetu mmoja kutoka Marekani na Uingereza tumezungumza naye watatusaidia vitabu na hivi karibuni tunatarajia kupokea vitabu vyengine, tutahakikisha kabla ya sherehe za Muungano au pengine katika sherehe za Muungano basi maktaba yetu tutaifungua na *Inshaallah* tutakualikeni Waheshimiwa sote tuhudhurie. Pengine

katika kikao cha Baraza kinachokuja tutafanya *timing* hizo ili tuweze kufungua wakati ule kwa vile waheshimiwa wote watakuwa wapo hapa.

Nakushukuru Mhe. Rashid Seif michango imekuwa *very constructive* umetusaidia, nadhani mengi nimeshayajibu na ushauri wako tumeuchukua pamoja na kusema kwamba Kengeja ni hali mbaya. Sio mbaya sana, lakini hairidhishi, tutajitahidi kuimarisha. Lakini unapofika wakati ukisema pale hata patasi inabidi tukaazime tena hawa watoto wanapasi vipi mitihani yao? Kweli nakiri kuna ukosefu wa vifaa na walimu wanajitahidi sana.

Mheshimiwa tutajitahidi kama patasi hizo kidogo tuziongeze, mimi nimekufahamu kwamba zipo, lakini hazitoshi kwa mahitaji ya pale, patasi na tupa. Tutajitahidi kuzitafuta tuongeze ili zitusaidie, lakini hapana kazi ya patasi na tupa tu pana na kazi nyengine vile vile ambazo tunahitajia kuzifanya. Mimi mwenyewe ninaguswa sana na chuo kile na Skuli ya Kengeja ya Ufundi, nitafurahi sana katika miaka hii miwili kufanya mabadiliko ya skuli yetu ile.

Mhe. Spika, suala la sayansi vile vile nimelieleza na *Inshaallah* kama nilivyokwishakulitolea ufafanuzi sina haja ya kulirejea tena. Vile vile kulikuwa na suala zima limejitokeza la uteuzi wa wanafunzi wa pale tutakaowapeleka. Hivi sasa sera yetu tunakubali kwamba wanafunzi wengi ukiwaambia wende Mbweni wanakataa, wale wa Lumumba waliopata *first class* kwenye *mathematics* na *physics* ukimwambia nenda Mbweni anakataa anakwambia mimi bora nisome hapa hapa. Tulikuwa na wakati tukalazimisha wende, lakini baadae tukajua hata haya masomo ya *chemistry, physics* tutakuja kupoteza vijana tukawa kidogo *flexible.*

Tatizo la mitihani ya Mbweni Chuo cha Karume ukifeli somo moja tu, basi inakuwa hadithi imemalizika, kweli unaweza uka-*suppliment* wakati mwengine lakini matokeo yake unaweza kuwa usibahatike moja kwa moja ikawa kazi yako ya miaka mitatu kukaa pale ni ya bure. Kwa hivyo, kinachofanyika sasa hivi wale wa Mikunguni wote na wanaotoka Kengeja wanaopata sifa za kuingia Chuo cha Karume wanakwenad Chuo cha Karume na wale ambao hawana sifa za kuingia *Form* V, basi waliopasi hesabu na *physics* angalau katika kiwango cha 'D' huwa tunawapeleka pale. Pana kazi kweli lazima tukiri.

Kwa hivyo, tutaliangalia hilo kutizama njia gani tufanye hasa tunapoelekea kwenye taasisi kama hii tuchukue wanafunzi wa aina gani. Kwa wale ambao watafanya vizuri sana tutajitahidi kuwapeleka kule katika masomo hayo ya *physics* na hesabu ili kuweza kukiimarisha chuo chetu. Sifa hizi kweli zina matatizo, lakini tutaziangalia zaidi na kuona kwa kiasi gani tunaweza kukifanya chuo kile.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi amezungumzia kwa ujumla na mimi nampongeza ushauri wake tumeupokea.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi amezungumza suala la upungufu wa vifaa vya kufundishia na walimu wenye sifa. Nimeshalitolea ufafanuzi wa kutosha, tuwe na *incentive* kwa walimu, tunaliangalia hilo sasa hivi wizarani kwa undani sana. Kumekuwa na malalamiko walimu wengi sana wale ambao wamesomesha miaka mingi wanashindwa na wanafunzi wao waliosomesha juzi tu kwa sababu wote wana sifa za diploma na wote wanapata mshahara wa aina moja. Kwa hivyo, na hilo pia tutaliangalia, hivi sasa tumo katika hatua nzuri ya maandalizi ya kutafuta muundo mpya wa watumishi wa walimu ili kuupeleka serikalini na walimu wajisikie vizuri.

Mhe. Ali Denge Makame mambo yako yalikuwa mazuri tumeyapokea na *Inshaallah* tutayaendeleza.

Mhe. Haji Faki Shaali ulianza kwa kusema kwamba dhamira ni nzuri lakini maandalizi je?

Sasa mimi nadhani umeshapata jawabu kwa kiasi fulani lakini kwa kiwango ambacho hatutafika mahali tukasema mia juu ya mia kila kitu kitakwenda vizuri. Tutapata mitihani ya hapa na pale lakini hatimaye tutafika pahali pazuri. Shahada na viwango vinakubalika kimataifa kabisa mwanafuzi yoyote anaye-*graduate SUZA* na Chuo cha Karume basi huyo anafaa popote pale duniani anakuwa na soko tu. Kwa hivyo, *qualification* tutaziangalia vizuri.

Suala jengine ulizungumzia suala zamani kulikuwa na Q*uarter Systerm* ya *University* sasa hivi imekwenda wapi haipo. Wakati ule tulikuwa hatuna *University* sasa zipo na sasa hivi hizi zetu hizi za nje zinakwenda kwa mujibu wa sifa fulani ndio utaingia kule. Kwa hivyo, wenye sifa hata kama watakuwa wengi kutoka Zanzibar basi wote wataingia. Lakini sifa zile kama huna basi huwezi kuendelea na masomo.

Pametolewa takwimu wote hapa na wengi wamezungumza kwamba bado tuna matatizo ya Sanyansi na Hesabu nalikubali hilo, *division* 1 zimekuwa kidogo. Lakini tunasema kidogo ukilinganisha na mwaka gani? Maana yake darasa la 12 mwaka huu waliopata *division 1* walikuwa wengi sana kuliko mwaka uliopota. Kidato cha kumi na nne kidogo mambo hayakuwa mazuri tunakubali mwaka huu lakini mwaka jana yalikuwa mazuri. Lakini haya ndio mambo yanavyokwenda na mitihani tusitarajie kila siku mambo yatakuwa mia juu ya mia. Lakini kila tukipata hivi ndio tunapata changamoto mpya ya kujirekebisha.

Nashukuru sana Waheshimiwa wote walisema kwamba Bajeti ya Elimu iongezwe. Sasa hivi tunapata karibu asilimia 20 ya Bajeti yote ya Serikali na tutafurahi sana kama tutaendelea kupatiwa bajeti hiyo na kuendeleza zaidi. Kwenye Miradi ya Maendeleo huko tulipata asilimia mia moja yaani pesa zote tulizotenga wakati ule karibu zote zile tulizipata. Natarajia na mwaka huu naomba mambo yanakwenda vizuri mpaka sasa hivi upatikanaji wa pesa unakwenda uzuri kwa hiyo miradi ya maendeleo mambo yanakwenda vizuri na hilo tutajitahidi kulisimamia vizuri zaidi ili kuhakikisha kwamba Bajeti ya Wizara ya Elimu inabakia kuwa ni kubwa.

Kweli wafanyakazi tulionao ni wengi na kwenye mambo mengine pesa nyingi zinakwenda katika maeneo hayo. Lakini na mambo mengine sasa hivi kuna hatua kwenye Bajeti ya Serikali.

Mhe. Assaa Othman Hamad naye vile vile alisema kuwa nia nzuri. Sasa akawa na mashaka mashaka ya Elimu ya Juu na mambo ya Muungano haya. Kama nilivyosema mwanzo haya ni ya juu lakini ya SMZ ni yetu wala msiwe na mashaka na tutaendelea kushirikiana na *Inshaallah* kuhakikisha kwamba tunaweka hadhi ya Elimu ya Juu na kuwa na sifa bora ziadi.

Vile vile katika masuala haya ya kuimarisha Elimu hii ya Ufundi nadhani nyote ni mashahidi. Mnajua kwamba tuna vituo viwili Mkokotoni na na Vitongaji pale na vifaa vinapelekwa na bado havijatosheleza lakini tutajitahidi kuvipeleka na vituo hivi vitafunguliwa popote pale.

Mhe. Assaa Othman Hamad aliuza huu uzoefu huu unatoka wapi. Unajua Mhe. Assaa Othman Hamad akichangia huwa na tabasamu humjui yuko katika hali gani anasema hii kaipata wapi Mhe. Waziri. Unajua sisi tuna wataalamu na pale Wizara ya Elimu tunafanyakazi kwa kushirikiana vizuri sana, haya masuala yote katika hatua za mwanzo mpaka imefika juu inawezekana kuna wazo lilitoka kwa njia moja au nyengine, lakini ni watendaji wenyewe wanakaa wanabuni na *Al-hamdulillah* kwa *brain* tulionazo pale wizarani kwa Wakuu wa Vyuo, Wakurugenzi, Katibu Mkuu na wasaidizi wake na Naibu Waziri mmemsikia hapa leo asubuhi alipokuwa anafanya muhtasari wa baadhi ya hoja, namshukuru sana. Kwa kweli, ananisadia na ni mtaalamu mzuri.

Kwa hivyo wataalamu hawa wamekaa wakaja na wazo hili kama tulivyokaa tukaja na wazo la kuanzisha *SUZA*, tumekaa sasa hivi Chuo cha Karume tutakaa sasa hivi tutasema Chuo cha Kiislam mambo yanakwenda kidogo kidogo. Huwezi kukaa katika ulimwengu huu ambao huwezi kubadika hapana wala usiogope katika kujaribu, jaribu uone na *Inshaalla* hatutofeli.

Benjamin Mkapa kule Pemba mnakumbuka vizuri tulikianzisha hata mimi mwenyewe nilipokianzisha nilikuwa nabahatisha jamani kweli lakini. Kwa bahati mwaka wa kwanza wamepasi mtihani kutoka Baraza la Mitihani, mwaka wa pili mia juu ya mia mwaka wa tatu mia juu ya mia, tukasema kumbe kulikuwa na uamuzi wa busara. Leo wanaendelea vizuri. Kwa hivyo, na haya mengine tutayaanzisha tutapata msukosuko wa hapa na pale lakini Mwenyezi Mungu atatusaidia. Kwa hivyo ghofu kweli ipo lakini naomba iondoshe imefika mahali ndipo na itashughulikiwa ipasavyo.

Mhe. Salum Hemed na yeye amechangia kwa kiasi kikubwa na alisema vile vile wazo ni zuri sana hakuna hata mjumbe mmoja aliyesimama akasema kwamba hili ni wazo baya na halifai kufanywa, wote walisema kuwa ni wazo zuri.

Mhe. Spika, sisi mawaziri tukipongezwa kama hivi huongeza kama kilo moja mbili, kwa hivyo huona mambo yetu yanakwenda vizuri. Lakini akisema Mjumbe na kusema kwamba hili wazo baya halifai tokeapo wembamba tunazidi kuwa wembaba. Lakini nashukuru kwa mswada huu *Al-hamdulillah* mambo yangu si mabaya.

Mhe. Spika, Mhe. Suleiman Hemed napenda nimtowe wasi wasi alisema hata hizi *other charges* hizi kuna matatizo hazipatikani. Mhe. Spika, pesa zinapatikana, kwa hali yetu zinapatikana kuliko tulipokuwa miaka mitano sita nyuma. Kulikuwa na wakati hapa miaka minne mitano pengine huko nyuma hizi *other charges* tunazitafuta, na huko nyuma kabisa mnakumbuka kabla ya mwaka 2000 mishahara miezi mitatu ndio tunapata. Leo *Alhamdullilah*, serikali hii ya Rais Amani Abeid Karume ikifika tarehe 20 au 21 watu wanaanza kupokea mishahara yao na tunaendelea kupata kwa wakati mpaka hii leo karibu miaka minne au mitano sasa hivi.

Pesa za miradi nimesema Wizara ya Elimu peke yake tulipata asilimia mia moja na wizara nyengine hivyo hivyo wamepata, lakini sijui wenyewe watajua wenyewe. *Other charges* vile vile Wakurugenzi wangu huko nyuma walikuwa wanalalamika hawana pesa za mafuta. Lakini sasa sijawaona karibu miaka miwili mitatu sijawaona ofisini kwangu kuja kunambia waziri hata pesa ya karatasi hatuna mambo yao yanakwenda vizuri na tunashukuru kazi zinakwenda uzuri kweli kweli nachukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe msiwe mbali si muda mkubwa Mhe. Waziri anamaliza ili tuweze kumaliza kazi hii.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Abdalla Juma nakushukuru sana lakini umesema Mikunguni imekufa iko hai bwana. Mikunguni madhubuti tena *alhamdullilah* pale pana mambo mazuri kweli ulikwenda zamani nakuomba sasa nenda. Skuli ile inatoa matokeo mazuri sana wanafanya kazi vizuri sana, tuwatieni moyo vijana wetu na sisi mtutie moyo unaposema kitu kimekufa unajua kuwa kimetoka roho. Mhe. Abdalla Juma nakuomba hili jambo la Mikunguni lipo na linaendelea vizuri. Sifa za Mwenyekiti hizi nisahazijatoa ufafanuzi sina haja tena ya kulirejea rejea.

Mhe. Haji Mkema na wewe tunakupongeza ushauri wako Mitaala hii tutaiangalia vizuri. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja ulipendekeza pale kwamba katika rufaa za wanafunzi basi Baraza isiwe ndio maamuzi ya mwisho. Ungehisi pengine waziri awe pale. Basi tutakaa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuliangalia hili kama tutaweza kulifanyia marekebisho.

Mhe. Omar Ali Jadi tunakushukuru sana kwa mchango wako majibu yake mengi tumeshayatoa wala usiwe na mashaka yoyote. Na nimekwambia kuwa Chuo chako cha kule Mchangamdogo kule kimo.

Mhe. Ame Mati pamoja na makofi unayopiga nakushukuru umetusaidia majengo yapo na tutaanzisha Mwenyezi Mungu akipenda wakati muafaka unapofika. Tutajitahidi kuimarisha zaidi zaidi suala zima la kuimarisha elimu hii ya Sayansi na mengineyo.

Mhe. Mzee Ali Ussi na wewe nakushukuru kwa mchango wako ulikuwa mzuri na *Inshalla* tuendelee kusaidiana.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman nakupa pongezi maalumu nakushukuru sana hali yako kama mtu wengine sasa hivi angekuwa kitandani kapumzika, kama vile tunaposema mzungu akipata mafua tu siku kumi hatoki ndani, sisi ukipata mafua ndio kwanza unafanya kazi unaingia huku na unakwenda na safari zako. Lakini umekaa mpaka Mhe. Spika, kakuonea huruma akakuamuru unaweza kukaa kitako. Lakini mchango wako tumeupata na nakuhakikishia kwamba tutalidhibiti vizuri suala hili na tutalisimamia. Nakushukuru sana umetupa moyo sana. Kwenye Sayansi tutaweka mkazo mzuri sana na wala tusiwe na matatizo yoyote, maandalizi yapo na tutajitahidi, na kwenye masuala ya ukurasa wa 223 uteuzi tutaliangalia.

Mhe. Ali Abdalla Ali najua uko, mchango wako ulikuwa mzuri ulitaka maelezo ya hapa n pale lakini mimi nadhani mengi nimeshayajibu kwa hivyo sina haja tena ya kuyasema. Kwa hivyo uamzi wa mwisho wa Baraza sisi waziri tutaliangalia hilo, sheria kuziangalia na kuzipitia.

Mhe. Zakiya Omar Juma kwa ujumla hayapo lakini nimesikia maelezo yake na tutayafanyia kazi.

Mhe. Naibu Waziri namshukuru, Mhe. Hamza Hassan Juma nakushuru sana na Mhe. Abass Juma Muhunzi na wewe nakushukuru sana nadhani na wewe majibu yako mengi nimeyajibu na tusiwe na wasi wasi mambo yatakaa sawa tukaei mkao wa kusoma tu mambo yote yamekamilika. Baada ya hayo naomba nichukue nafasi vile vile kwa niaba ya wananchi wa Makunduchi kuunga mkono mswada huu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa na kuamuliwa)

(Hoja iliamuwa na Kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza zima ili kupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Kifungu cha 1 Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 2 Marekebisho yake na tafsiri
Kifungu cha 3 Uanzishwaji wa Taasisi
Kifungu cha 4 Idara za Taasisi
Kifungu cha 5 Kazi za Taasisi
Kifungu cha 6 Marekebisho yake Baraza la Taasisi
Kifungu cha 7 Uwezo wa Baraza
Kifungu cha 8 Bodi ya Taaluma
Kifungu cha 9 Marekebisho yake Mikutano ya Baraza
Kifungu cha 10 Uteuzi wa Mkurugenzi
Kifungu cha 11 Na marekebisho yake uteuzi wa Mrajisi
Kifungu cha 12 Uajiri wa wafanyakazi
Kifungu cha 13 Jumuiya ya wanafunzi
Kifungu cha 14 Fedha za Taasisi
Kifungu cha 15 Uwekezaji wa Fedha za Taasisi
Kifungu cha 16 Makisio ya Fedha
Kifungu cha 17 Hesabu za Taasisi na Ukaguzi
Kifungu cha 18 Ripoti ya Matumizi ya Fedha kupelekewa Baraza la Wawakilishi
Kifungu cha 19 Sheria ndogo ndogo
Kifungu cha 20 Uchunguzi wa kosa la Kinidhamu
Kifungu cha 21 Rufaa
Kifungu cha 22 Kubakiza
Kifungu cha 23 Kanuni pamoja na Marekebisho yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza zima umeupitia mswada wangu kifungu baada ya kifungu na kukubali pamoja na mashahihisho, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mswada wa kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia Zanzibar ya 2008
(Kusomwa kwa mara Pili)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria kuanzishwa kwa Taasisi ya Karume ya Sayansi ya Teknolojia mwaka 2008 usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Waziri wa Nch (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Spika: Naona tumekubaliana shughuli nyengine zianze kesho. Sasa namwita Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi.

KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi kwa kuwa Mhe. Waziri wa Elimu amefanya kazi kubwa leo hapa itabidi tukampumzishe. Naomba kutoa hoja kwamba uliahirishe Baraza lako tukufu kabla ya wakati wake mpaka kesho siku ya Jumanne saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, naafiki.
(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Saa 12:20 Jioni Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 27/01/2009 Saa 3:00 asubuhi)